

SHERIA ZA HABARI NCHINI TANZANIA:

Mwongozo kwa Watendaji



*Mtiririko wa Machapisho kwa
Wadau wa Maendeleo*

SHERIA ZA HABARI NCHINI TANZANIA

Mwongozo kwa Watendaji



*Mtiririko wa Machapisho kwa
Wadau wa Maendeleo*

Kimechapishwa Julai 2019

Kuhusu Boresha Habari

Boresha Habari ni mradi unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) nchini Tanzania kupitia msaa chini ya mradi unaoendeshwa chini ya makubaliano maalum ya ushirikiano wa taasisi za Strengthening Civil Support Globally (SCS), Leader with Associates (LWA). Boresha Habari unalenga kuimarisha jitihada za kuleta uwazi na kuweka mazingira wezeshi kwa vyombo vya habari na asasi za kiraia nchini Tanzania kutoa taarifa sahihi na yakinifu katika kuendeleza ushiriki, ujumuishi na uwajibikaji.

Kuhusu ICNL

Taasisi ya International Center for Not-for-Profit Law (ICNL) hufanya kazi na serikali, asasi za kiraia, na jumua ya kimataifa kwenye nchi zaidi ya 100 ili kuboresha mazingira ya kisheria kwa asasi za kiraia, misaada ya kibinadamu, na ushiriki wa wananchi duniani kote. Ikiwa imejikita zaidi kwenye kanuni za jumla na utamaduni wa sheria za kimataifa, dhima ya ICNL inahusisha kulinda na kuendeleza maeneo haya yaliyotajwa. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu kazi za ICNL kupitia tovuti yao: www.icnl.org.

Kuhusu Internews

Taasisi ya Internews inawezesha watu duniani kote kupitia habari na taarifa za kuuminika, na zenye ubora wa hali ya juu wanazohitaji ili kuweza kufanya maamuzi sahihi, kushiriki katika shughuli mbalimbali kwenye jamii zao, na kuwajibisha mamlaka zilizo. Taasisi ya Internews inalenga kuwawezesha watu duniani kujipambanua kwa kutumia njia ya kufahamu, kutafuta na kupata taarifa sahihi. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu kazi za Internews kupitia tovuti yao: www.internews.org.

Kuhusu FHI 360

Shirika la FHI 360 ni taasisi ya kimataifa isiyoye kiserikali inayofanya kazi kwa lengo la kuboresha afya na ustawi wa watu nchini Marekani na duniani kwa ujumla. FHI hushirikiana na serikali, sekta binafsi, na asasi za kijamii kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii ili kutoa huduma za afya zitakazosaidia kuokoa maisha ya watu mbalimbali, kuboresha elimu, na kutoa fursa kwa watu kuweza kushiriki kwenye shughuli za kiuchumi. Unaweza kujifunza zaidi kuhusu kazi za FHI kupitia tovuti yao: www.fhi360.org.

Shukrani

Kitabu hiki ni matokeo ya jitihada, uzoefu, na weledi wa watu mbalimbali. Shukrani za pekee ziende kwa ICNL kwa kuwa mstari wa mbele katika jitihada hizo, ikishirikiana na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Chama cha Wanahabari wa Kusini mwa Afrika tawi la Tanzania (MISA-TZ). Shukrani za pekee ziende kwa Angela Nicoara na Wenceslaus Mushi wa Internews kwa msaa wao katika kufanya marejeo na uhari.

Timu ya Uhariri

Maudhui: Zach Lampell, Aloys Habimana, Lily Liu, na Waruguru Kaguongo, ICNL;

Kajubi Mukajanga na Humphrey Mtuy, MCT; na Gasirigwa Sengiyumva, MISA-TZ

Uhariri: Irene Petras na Catherine Shea, ICNL

Ubunifu: Emily Honstein Stanton na Jeff Vize, ICNL

Jalada: Design Lab 360, FHI 360

Kitabu hiki kimeandaliwa kwa lengo la kufikisha taarifa pekee, na sio mbadala wa ushauri wa kisheria. Sheria zinaweza kubadilika, na fasili ya sheria inaweza kutofautiana kati ya mtu mmoja na mwingine. Waandishi wa kitabu hiki hawawajibiki kwa namna yoyote ile kwa mabadiliko, tofauti, au usahihi wa taarifa zilizo.

Kitabu hiki kimewezeshwa kwa ufadhili wa Watu wa Marekani kupitia Uwakilishi wa USAID nchini Tanzania chini ya masharti ya mkataba AID-621-LA-17-00001. Waandishi wanawajibika kwa maudhui ya kitabu hiki, pia, maudhui hayo hayawakilishi mawazo ya USAID au Serikali ya Marekani.

© 2019. Haki zote zimehifadhiwa na FHI 360, Internews, ICNL na USAID au Serikali ya Marekani. Kitabu hiki kinaweza kunukuliwa, kunakiliwa, au kuchukuliwa katika sehemu ndogo au kwa utimilifu wake, kwa kuzingatia masharti ya kukisambaza bila ya gharama yoyote na kwa mtumiaji na kutambua taasisi za ICNL, Internews, FHI 360 na USAID.

YALIYOMO



SURA YA I

UTANGULIZI NA UKTADHA

3



SURA YA II

MISINGI YA KISERA NA NA KISHERIA
INAYOSIMAMIA TASNIA YA HABARI KIMATAIFA

8



SURA YA III

MISINGI YA KISERA NA KISHERIA
INAYOSIMAMIA TASNIA YA HABARI KITAIFA

18



SURA YA IV

KUPAMBANUA MISINGI YA KISHERIA -
KINGA NA MIKAKATI

67



SURA YA V

REJEA MUHIMU

84

VIFUPISHO

ACHPR	African Commission on Human and Peoples' Rights (Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Umoja wa Afrika)
AU	African Union (Umoja wa Afrika)
CSO	Civil Society Organization (Asasi ya/za Kiraia)
DNS	Domain Name Service (Jina Tofauti la Utambulisho Mtandaoni)
EAC	East African Community (Jumuia ya Afrika Mashariki)
HRD	Human Rights Defender (Watetezi wa Haki za Binadamu)
ICCPR	International Covenant on Civil and Political Rights (Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa)
ICT	Information and Communication Technologies (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano – TEHAMA)
LHRC	Legal and Human Rights Centre (Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu)
NBS	National Bureau of Statistics (Ofisi ya Taifa ya Takwimu)
NGO	Non-Governmental Organization (Taasisi Zisizo za Kiserikali)
NSS	National Statistics System (Mfumo wa Taifa wa Takwimu)
OAS	Organization of American States (Umoja wa Nchi za Bara la Amerika)
OSCE	Organization for Security and Co-operation in Europe (Mwakilishi wa Shirika la Usalama na Ushirikiano la Ulaya)
TBC	Tanzania Broadcasting Corporation (Shirika la Utangazaji Tanzania)
TCRA	Tanzania Communications Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania)
TISS	Tanzania Intelligence and Security Service (Idara ya Usalama wa Taifa)
UDHR	Universal Declaration of Human Rights (Tamko la Kimataifa ya Haki za Binadamu)
UN	United Nations (Umoja wa Mataifa)
UPR	Universal Periodic Review (Mapitio Jumuishi Maalum ya Haki za Binadamu)
VPN	Virtual Private Network (Mtandao Binafsi)

SURA YA I

UTANGULIZI NA MUKTADHA



Kitabu hiki kinalenga kusaidia watendaji katika tasnia ya habari, watetezi wa haki za binadamu, na asasi za kiraia nchini Tanzania kuelewa misingi ya kisheria na kisera inayohusiana na shughuli zao za kila siku.

Tasnia ya habari nchini Tanzania inakabiliwa na changamoto nyingi zinazoathiri moja kwa moja dhima yake ya kuendeleza demokrasia, utawala bora na uwajibikaji. Katika miaka mitatu iliyopita, Tanzania imetunga sheria kadhaa zinazoia uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kujieleza, uhuru wa kujieleza, na zinazokazia ukali wa sheria zilizopo ambazo ni vikwazo katika kuhabarisha wananchi. Kwa pamoja, sheria hizi zinajinaisha uandishi wa habari za kina na za uchunguzi.

Vitendo vya uvunjifu wa uhuru wa habari vimeongezeka hivi karibuni vikihusisha vitisho, mashambulio, na kutekwa kwa waandishi wa habari, uchomaji moto na uharibifu wa vifaa vya kazi vinavyotumiwa na waandishi wa habari. Vyombo vingi vya habari vimeadhibiwa kwa kutozwa faini, kusimamishwa kwa muda au kufungiwa kabisa kwa kukiuka kanuni za maudhui, huku nyingi ya adhabu hizo zikitolewa mwaka 2016 Magazeti kadhaa yakiwemo Mawio, Mwanahalisi na Raia Mwema yamesitishwa kwa kuchapisha habari zinazokosoa utawala wa sasa na awamu za zamani za Serikali ya Tanzania, huku waandishi wakishitakiwa kwa uchochezi na kuchapisha



taarifa za uongo. Mwaka 2017, Serikali ilisitisha utamaduni uliodumu kwa takriban miaka ishirini wa kutangaza moja kwa moja shughuli za Bunge kwa kisingizio cha Shirika la Utangazaji la Taifa lisingeweza kushindwa kumudu gharama za kurusha matangazo hayo.

Baadaye, Serikali ilipanua wigo wa katazo hilo hadi kuvihusisha vyombo binafsi vya habari, pamoja na vyombo hivyo kutokuwa na changamoto za kifedha.

Vikwazo vimewagusa hadi wachapishaji na wasambazaji wa habari mitandaoni, huku mwanzilishi wa mtandao maarufu wa kupashana habari na kufichua maovu wa Jamii Forums akishitakiwa kwa kukataa kueleza vyanzo vya taarifa anazochapisha. Vyombo mbalimbali vya habari vimeadhibiwa kwa kutakiwa kulipa kubwa kwa kuchapisha na kusambaza maudhui ya ripoti ya uangalizi wa uchaguzi iliyoandaliwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, ambayo ilionesha dukuduku kuhusu ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi uliohusisha jeshi la polisi na baadhi ya wagombea. Madhara ya vitisho hivyo ni pamoja vyombo vya habari kuogopa kuripoti kuhusu shughuli muhimu za asasi za kijamii, hivyo asasi hizo kushindwa kuarifu wadau wake na jamii kwa ujumla kuhusu shughuli zao, au kutoa taarifa mbadala wa zile zinazotolewana upande wa Serikali na taasisi zake.

Mazingira hayo ya woga kwenye tasnia ya habari pia yanachochewa na matamko ya kisiasa yanayovionya vyombo vya habari kutotoa taarifa zinazodaiwa kuhujumu juhudi zinazolenga kuleta maendeleo nchini humo.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye vyombo vingi zaidi vya habari Afrika Mashariki. Hata hivyo, vyombo vingi



kati ya hivyo ni vidogo, havina rasilimali za kutosha, dhaifu, na ambavyo waandishi wake wa habari hukutana na changamoto mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao ya kitaaluma na katika kuhakikisha kwamba wanatoa habari zenye uyaakinifu (objectivity), yaani zisizoegemea upande wowote. Pia, uamuzi wa Serikali wa kupeleka matangazo yake na ya taasisi zake mbalimbali kwa vyombo vya habari vya Serikali pekee na vile visivyoikosoa unaathiri uhai wa vyombo binafsi vya habari.

Hata hivyo, Tanzania sio nchi pekee inayofanya hivyo; mwenendo wa sasa wa kisiasa duniani kote unaashiria kusinyaa kwa demokrasia, hasa uhuru wa habari na haki kuwasiliana.

Waandishi wa habari, watetezi wa haki za binadamu na asasi za kiraia hawana budi kufahamu ipasavyo muktadha wa kisheria unaosimamia shughuli za uandishi wa habari, na mbinu zinazoweza kuwasaidia kutekeleza majukumu yao katika mazingira yaliyopo.

Kitabu hiki kinalenga:

- Kufafanua dhima na majukumu ya waandishi wa habari kwa mtazamo wa haki za binadamu;
- Kueleza misingi ya kisheria na kisera inayosimamia tasnia ya habari nchini Tanzania, na;
- Kutoa mapendekezo kuhusu namna ya kufanya kazi ya uandishi wa habari kwa kuzingatia changamoto za mazingira ya sasa.



UHUSIANO KATI YA TASNIA YA HABARI NA DHANA YA HAKI ZA BINADAMU

Demokrasiasahihihutegemea uhuru wavyombo vya habari vinavyoweza kusimamia maslahi ya jamii. Kimsingi, haki zinazohusiana na uhuru wa kutoa maoni na kujieleza bila ya kuingiliwa, kutafuta, kupokea, na kusambaza taarifa na mawazo ya aina mbalimbali kwa kufuata kanuni chache zilizowekwa, ni haki inayotambuliwa na sheria za kimataifa. Vyombo huru vya habari ni msingi muhimu wa kuhakikisha kupatikana kwa uhuru na haki hizi.

Katika kuhakikisha hilo, dhima ya waandishi wa habari ni zaidi ya kazi yao; uandishi ni taaluma inayoweza kusaidia kupatikana kwa mitazamo na maoni ya aina mbalimbali kwenye nchi.

Vyombo vya habari hutoa fursa kwa watu kuhabarishwa na wao kuweza kujenga na kueleza mitazamo yao.

Tasnia imara ya habari huwezesha jitihada za kushawishi kupatikana kwa hoja mpya na mabadiliko muhimu, na kufuatilia utendaji wa Serikali ili kuifanya iwajibike kwa wananchi wake.

Waandishi wa habari hutegemea taarifa kutoka kwenye vyombo na taasisi mbalimbali, na vyanzo vinavyoaminika (wakiwemo wafichua uhalifu mbalimbali) ili kuandaa habari na kuiarifu jamii. Sheria zinazoweza (kuliko kuzuia) juhudi hizo ni muhimu katika utendaji wa waandishi na kushamiri kwa tasnia nzima ya habari.

Kwa upande wao, waandishi wa habari na watendaji



wengine kwenye vyombo vya habari wana wajuu wa kuhakikisha kwamba wanafuata misingi na maadili ya taaluma zao katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Hii ni pamoja na kutoa taarifa za uhakika, kufuata kanuni zote za maadili, na kuhakikisha uhuru wa kiutendaji kwenye tasnia ya habari.

SURA YA II

MISINGI YA KISERA NA KISHERIA
INAYOSIMAMIA TASNIA YA HABARI KIMATAIFA



Mikataba mbalimbali ya kimataifa, bara na kanda inalinda tasnia ya habari, waandishi wa habari, na watetezi wa haki za binadamu kutoingiliwa na Serikali. Mikataba hiyo inaweka wajibu kwa Serikali kufuata, kuendeleza, na kulinda uhuru wa kutoa maoni na kujieleza.

MIKATABA YA KIMATAIFA

TAMKO LA KIMATAIFA LA HAKI ZA BINADAMU
(UDHR)

Kifungu cha 19 cha Tamko hilo kinasema: Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza; haki hii pia inahusisha uhuru wa mtu kuamini katika maoni yake bila kuingiliwa kwa namna yoyote, na uhuru wa kutafuta na kusambaza taarifa, maoni na mawazo yake kwa njia yoyote bila ya kujali mipaka.

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na
Kisiasa (ICCPR)

Tanzania imeridhia mkataba huu mwaka 1976, na hivyo inawajibika kisheria kufuata masharti ya mkataba huo. Kifungu cha 19 cha mkataba huo kinazungumzia uhuru na haki ya kujieleza:

- 1. Kila mtu atakuwa na haki ya kuwa na maoni na kuyaamini maoni hayo bila ya kuingiliwa kwa namna yoyote.*
- 2. Kila mtu atakuwa na haki na uhuru wa kujieleza; haki hii itahusisha mtu kutafuta, kupokea, na kusambaza taarifa*



na mawazo ya aina mbalimbali, kwa njia ya mdomo au maandishi, na bila ya kujali mipaka, kwa kuandika au kuchapisha, kwa njia ya sanaa, au njia nyingine yoyote atakayoichagua.

3. Utekelezaji wa haki zilizoainishwa kwenye aya ya 2 ya kifungu hiki kinaendana wajibu na majukumu maalum. Kwa hivyo, haki hiyo inaweza kuhusisha vikwazo mbalimbali, hata ambavyo ni vya muhimu na vitawekwa kwa mujibu wa sheria:

(a) Vinavyolenga kulinda haki na heshima ya watu wengine;

(b) Vinavyolenga kulinda usalama wa nchi au utulivu wa kijamii, au afya na maadili ya jamii.

Haki ya uhuru wa kujieleza inahusisha kuchambua, kujadili kwa uwazi, kutoa kauli zinayoweza kukwaza, kushitua, kusumbua na kukosoa wengine.

Vikwazo: Jaribio la Sehemu Tatu

Vikwazo kwa uhuru wa kujieleza vilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 19 vitakubalika kisheria iwapo vitakidhi masharti ya jaribio jumuishi lenye sehemu tatu, kama ilivyooneshwa kwenye Kifungu cha 19(3). Kwa mujibu wa jaribio hili:

1. Kikwazo chochote ni lazima kiwekwe kwa mujibu wa sheria, ambayo iko wazi na inayoweza kuonwa na kila mtu (*kanuni za uwazi na kutabirika*);

2. Kikwazo chochote ni sharti kiendane na moja kati ya malengo ya Kifungu cha 19(3), amabyo ni:

a. kulinda haki na heshima ya watu wengine;

b. kulinda usalama wa nchi au utulivu wa kijamii,



au afya na maadili ya jamii (*kanini ya uhalali*); na

3. Kiwazo chochote ni sharti kithibitike umuhimu wake na kihusishe vikwazo vichache katika kufikia lengo lililokusudiwa (*kanuni za uwiano na umuhimu*).

Kanuni za uwazi na kutabirika: kikwazo chochote kwa uhuru wa kujieleza ni shari kiwekwe kwa kuzingatia misingi ya kisheria. Sheria hiyo ni lazima ieleze kinagaubaga, ili kufanya mamlaka za Serikali na wananchi waelewe aina ya maoni yanayoruhsiswa na inayokatazwa.

Wananchi ni lazima waweze kudhibiti mienendo yao ili kuendana na matakwa ya sheria.

Kanuni ya uwiano na umuhimu: kikwazo chochote kwa uhuru wa kujieleza ni lazima kiweke masharti machache kwa kadiri iwezekanavyo, na adhabu yoyote itakayowekwa kwa kukiuka sheria hiyo ni lazima izingatie busara na iwiane na madhara yanayosababishwa na kitendo husika. Kwa mfano, chini ya sheria za kimataifa, adhabu ya kifungo kwa kosa la kukashifu haiwiani na kosa husika, na hivyo haikidhi vigezo vya jaribio hili lenye sehemu tatu.

Miundo Huru ya Umoja wa Mataifa na Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Umoja wa Afrika (ACHPR)

Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa iliyoundwa chini ya ICCPR ili kusimamia utekelezaji wa Mkatoba huo, katika Ufafanuzi wa Jumla Na. 34 inafafanua maudhui ya haki ya uhuru wa kujieleza na kutoa maoni, pamoja na majukumu ya Dola katika kuhakikisha upatikanaji wa haki hiyo. Kila nchi (dola) ina wajibu wa kutoa taarifa ya namna inavyotekeleza matakwa haya ya kimataifa. Tume



hii pia hutoa Mahitimisho ya Jumla ili kusaidia nchi katika kutekeleza matakwa ya Mkataba huo wa ICCPR.

Waangalizi Maalum wa Umoja wa Mataifa na Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Umoja wa Afrika hutoa taarifa na kushauri kuhusu masuala maalum ya haki za binadamu ya nchi wanazoshughulikia kwa kufata dhima ama mtazamo wa nchi husika, na kuchangia kwenye kushamiri kwa misingi ya haki za binadamu kwenye nchi hizo. Waangalizi hao hutekeleza jukumu hili kwa kuzuru nchi husika, kuandika taarifa zinazotokana na ziara hizo, pamoja na kuandika taarifa za dhima mahususi.

Taarifa hizo za Waangalizi Maalum ni muhimu katika kuweka kumbukumbu za mienendo, maendeleo na changamoto za kuhakikisha upatikanaji wa haki za binadamu, na katika kutoa mapendekezo ya namna kuendeleza na kulinda haki za binadamu.

Waangalizi Maalum wa haki na uhuru wa kutoa maoni na kujieleza wamefafanua kanuni na vigezo mbalimbali kwa changamoto zinazosababishwa na mazingira kwamishi ya kisheria kwa tasnia ya habari nchini Tanzania. Wataalam huru wanne, ambao ni (i) Mwangalizi Maalum wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Uhuru wa Kujieleza na Kutoa Maoni, (ii) Mwangalizi Maalum wa Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Umoja wa Afrika Kuhusu Uhuru wa Kujieleza na Kupata Taarifa, (iii) Mwakilishi wa Shirika la Usalama na Ushirikiano la Ulaya (OSCE) Kuhusu Uhuru wa Vyombo vya Habari; na (iv) Mwangalizi Maalum wa Umoja wa Nchi za Bara la Amerika (OAS) Kuhusu Uhuru wa Kujieleza wametoa matamko mbalimbali ya pamoja kuhusu uhuru wa kujieleza. Baadhi ya kanuni hizo ni kama



zinavyooneswa hapa chini:

- Nchi mbalimbali zina wajibu wa kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa na mawazo, jukumu linalohusisha pia kutunga sheria zitakazosimamia haki ya kupata taarifa, kulinda wafichua uhalifu, kushughulikia kashfa kwa kutumia sheria za madai badala ya za jinai, na zisizotoa fidia kubwa kupita uhalisia katika maisha ya kawaida. (Tamko la Tarehe 2 Mei 2018).
- Katika kudhibiti maudhui ya mtandaoni, nchi zina wajibu wa kuzuia baadhi tu ya maudhui hayo, kama vile picha au maelezo yanayohusu ngono zinazohusisha watoto wadogo, na kauli zinazochochua chuki, ugaidi au mauaji ya kimbari.
- Makatazo ya jumla kuhusu kusambaza habari kwa kutumia kauli butu, tata na zisizotoa ufafanuzi kama vile (habari za uongo” au “taarifa isiyo na uyaakinifu” yanapaswa kukomeshwa. (Tamko la Tarehe 3 Machi 2017).
- Sheria za jinai zinazoshughulikia kashfa ni kikwazo na hazina budi kuondolewa. (Tamko la Tarehe 3 Machi 2017).
- Kuhusu habari za kwenye mtandao wa intaneti, mawakala (wakiwemo waandishi wa habari na vyombo vya habari) hawastahili kuwajibishwa kwa habari au taarifa yoyote



iliyoandaliwa, kutangazwa au kuchapishwa na chombo au mtu mwingine, isipokuwa tu iwapo wataingilia maudhui ya habari hiyo, watakaidi amri halali ya mahakama kuondoa maudhui hayo, na wana uwezo wa kuondoa kitaalam wa kufanya hivyo. (Tamko la Tarehe 3 Machi 2017).

- Hitaji la kusajili au kutoa leseni kwa mwandishi mmoja mmoja ni kinyume na haki ya uhuru wa kujieleza. Hitaji hilo litakuwa sahihi pale tu wanahabari watakapohitaji kupewa ruhusa ya kuingia sehemu au kwenda kuhudhuria matukio maalum. Kunastahili kuundwa chombo huru kitakachosimamia kwa haki na kwa uwazi, mchakato wa kutoa vibali, na vigezo vya utoaji wa vibali hivyo bila ya kuonesha ubaguzi wa namna yoyote vichapishwe na kuwekwa wazi ili vifahamike na kila mtu mapema iwezekanavyo kabla ya kuombwa kwa vibali husika. (Tamko la Tarehe 18 Disemba 2003).
- Mamlaka za umma za udhibiti wa tasnia ya habari zilindwe dhidi ya kuingiliwa kisiasa au kiuchumi, ikiwemo uteuzi wa wanachama, mchakato unaolazimu kuhusisha ushiriki mpana wa jamii na usiostahili kuingiliwa kwa namna yoyote ile na chama cha siasa. (Tamko la Tarehe 18 Disemba 2003).



MIKATABA YA BARANI AFRIKA

Mkataba wa Haki za Binadamu na Haki za Watu wa Umoja wa Afrika (Mkataba wa Afrika)

Kifungu cha 9 cha Mkataba wa Afrika kinalinda haki ya uhuru wa kujieleza na kutoa maoni:

- 1. Kila mtu atakuwa na haki ya kupokea taarifa.*
- 2. Kila mtu atakuwa na haki ya kujieleza na kusambaza mawazo yake kwa kuzingatia misingi ya sheria.*

Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Umoja wa Afrika (ACHPR) ina wajibu wa kufasiri Mkataba huo. Tume hiyo imekuwa ikitekeleza wajibu huo kwa namna mbalimbali, ikiwemo njia ya kutoa Maazimio na Matamko.

Maazimio na Matamko ya Msingi ya ACHPR:

Azimio Kuhusu Haki ya Uhuru wa Taarifa na Kujieleza Kupitia Teknolojia ya Intaneti Barani Afrika (lilikubaliwa Tarehe 4 Novemba 2016): Nchi zilizoridhia Mkataba wa Afrika hazina budi kutunga sheria zitakazohakikisha kupatikana, kuheshimu na kulinda haki ya wananchi ya uhuru wa taarifa na kujieleza kwa kupitia teknolojia ya intaneti.

Azimio Kuhusu Usalama wa Waandishi na Watendaji Wengine wa Tasnia ya Habari (lilikubaliwa Tarehe 12 Mei 2011): Nchi (na mamlaka zake husika) zilizoridhia Mkataba wa Afrika hazina budi kutekeleza wajibu wao wa kuzuia na kuchunguza matukio yote ya uhalifu dhidi ya waandishi au watendaji wengine wa tasnia ya habari na kuwashughulikia wahusika wote waliofanya vitendo hivyo kwa mujibu wa sheria.



Pande zote zinazohusika kwenye mapigano au migogoro inayohusisha matumizi ya silaha zina wajibu wa kuheshimu uhuru wa wanahabari kutekeleza majukumu yao ya kitaaluma, pia zina wajibu wa kuhakikisha usalama wa waandishi na watendaji wengine kwenye tasnia ya habari kwa mujibu wa sheria za kimataifa za masuala ya kiutu.

Azimio Kuhusu Kudorora kwa Uhuru wa Kujiieleza na Kupata Taarifa Barani Afrika (lilikubaliwa Tarehe 26 Mei 2010): Nchi zilizoridhia Mkataba wa Afrika zina wajibu wa kutunga sheria ili kulinda haki ya uhuru wa kujiieleza na kupata taarifa. Sheria hizo ni sharti ziongozwe na kanuni za kimataifa na zile za barani Afrika, zinazolenga kuzuia ukiukwaji wa haki hizi.

Nchi zina jukumu la kufanya uchunguzi wa ukiukwaji wowote wa haki hizi, hasa vifo vya waandishi wa habari waliowekwa kizuizini, na kuwafikisha wahusika kwenye vyombo vya sheria.

Tamko Kuhusu Kanuni Misingi ya Uhuru wa Kujiieleza barani Afrika (lilikubaliwa mwaka 2002): Nchi zilizoridhia Mkataba wa Afrika zina wajibu wa kuhakikisha kupatikana kwa uhuru wa kujiieleza na kupata taarifa, ambao pia unahusisha haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa na mawazo ya aina mbalimbali kwa njia ya mdomo au maandishi, na bila ya kujali mipaka, kwa kuandika au kuchapisha, kwa njia ya sanaa, au njia nyingine yoyote atakayoichagua, hata kama ni nje ya mipaka ya nchi. Tamko hili linafafanua misingi mbalimbali, ikiwemo:

- A diverse, independent private broadcasting sector rather than a State monopoly, which



is Kuwapo kwa tasnia ya utangazaji habari yenye washiriki wa aina mbalimbali, vyombo huru vinavyomilikiwa na watu au taasisi binafsi, kuliko kuwapo kwa ukiritimba wa Dola (Serikali), ambao ni kinyume cha kuwapo kwa uhuru wa kujieleza.

- Uwajibikaji wa vyombo vya utangazaji vya umma kwa wananchi kupitia muhimili wa kutunga sheria (Bunge), kuliko muhimili wa utawala.
- Mamlaka huru za udhibiti wa vyombo vya utangazaji na mawasiliano ya simu, zinazolindwa ipasavyo dhidi ya kuingiliwa kwenye utendaji wao kisiasa au kiuchumi.
- Mtumo wa usajili wa magazeti na machapisho mengineyo usioweka vikwazo dhidi ya uhuru wa kujieleza.
- Sheria dhidi ya kashfa zisizozuia usambazaji wa habari au taarifa zenye maslahi mapana kwa jamii.
- Kulinda vyanzo vya habari au taarifa za siri isipokuwa katika mazingira maalum yaliyoainishwa.



MIKATABA YA KIKANDA – AFRIKA MASHARIKI

Mkataba wa Kuundwa kwa Jumuaia ya Afrika Mashariki

Mkataba huu unaunda Jumuaia ya Afrika Mshariki. Nchi zilizoridhia Mkataba huu zina wajibu wa kuendeleza kanuni za msingi za za Jumuaia hii, kama inayooneshwa kwenye Kifungu cha 6(d), kinachosisitiza “utawala bora, ukiwemo kuheshimu na kufuata misingi ya demokrasia, utawala wa sheria, uwajibikaji, uwazi, pamoja na kutambua na kulinda haki za watu na za binadamu.”

SURA YA III

MISINGI YA KISERA NA KISHERIA
INAYOHUSU TASNIA YA HABARI KITAIFA



KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalinda uhuru wa kujieleza, japokuwa haielezi moja kwa moja kuhusu uhuru wa vyombo vya habari:

Kila mtu -

(a) ana uhuru wa kuwa na maoni na kujieleza maoni au mawazo yake;

(b) ana haki ya kutafuta, kupokea na, au kusambaza taarifa bila ya kujali mipaka ya nchi;

(c) ana uhuru wa kuwasiliana na haki ya kulindwa dhidi ya kuingiliwa kati kwa mawasiliano yake; na

(d) ana haki ya kupata taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu yanayoendelea kuhusu maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii.

Mipaka

Haki hizi za Kikatiba, ikiwemo Ibara ya 18, hazitatumiwa au kutekelezwa na mtu mmoja kwa namna ambayo itazuia au kuingilia kati uhuru wa watu wengine, au maslahi ya umma (Ibara 30(1)). Haki hizi zinzaweza kuzuiwa kwa sababu mbalimbali:



- Kuhakikisha ulinzi, usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii, afya ya jamii, mipango ya maendeleo ya miji na vijiji, ukuzaji na matumizi ya madini au ukuzaji na uendelezaji wa mali au maslahi mengineyo yoyote kwa nia ya kukuza manufaa ya umma; au
- Kulinda heshima, haki na uhuru wa watu wengine au faragha ya watu wanaohusika shauri lolote mahakamani, kuzuia kutoa habari za siri, au kutunza heshima, mamlaka na uhuru wa mahakama.

Muhimu: Masharti haya ni mapana kuliko yaliyoainishwa kwenye Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR). Kwa kuzingatia maudhui ya Katiba, kanuni za uwiano na umuhimu hazipewi uzito unaostahili kama vigezo muhimu katika kuzuia haki hizi za msingi.

SHERIA ZA NCHI ZA UDHIBITI WA VYOMBO VYA HABARI

Sheria ya Huduma za Habari, 2016

Sheria ya Huduma za Habari inasimamia weledi katika tasnia ya habari, na inaunda Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari, na Habari na misingi mingine ya udhibiti wa tasnia ya habari.

Vipengele muhimu na athari zake kwa tasnia ya habari ni pamoja na:

Usajili na Ithibati:

- Vyombo vya habari vya uchapishaji (magazeti) vinalazimika kupata leseni kutoka kwa



Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo. Kifungu cha 8-10 vinaeleza mchakato wa kuomba, kukataliwa, na kufutwa kwa maombi ya leseni. Mamlaka ya rufaa dhidi ya maamuzi hayo yapo chini ya Waziri mwenye dhamana ya maudhui na rufaa inalazimika kuwasilishwa ndani ya siku thelethini baada ya kutolewa kwa uamuzi husika.

- Sheria hii pia inaweka masharti ya mwandishi wa habari kuthibitishwa (kupata ithibati) ili kufanya kazi za uandishi. [Kifungu cha 19] Bodi inaweza kufuta uthibitisho wa mwanahabari kutokana na kukiuka kwa kiasi kikubwa maadili ya taaluma yaliyoainishwa katika kanuni za maadili ya taaluma ya uandishi wa habari, na kwa mwandishi wahabari asiye raia wa Tanzania, kutotekeleza lengo la uthibitisho wake. Bodi hutunza orodha ya wanahabari ikijumuisha majina na maelezo ya wanahabari waliothibitishwa.
- Mwandishi ambaye jina lake limeondolewa kutoka kwenye Orodha ya Wanahabari au aliyesimamishwa kufanya kazi za uandishi wa habari hatofanya kazi hizo walau kwa muda wa miezi mitatu. Mamlaka ya rufaa dhidi ya maamuzi hayo yapo chini ya Waziri na Mahakama Kuu. [Kifungu cha 21]

Athari: Hitaji la kisheria la kusajili na kutoa ithibati kwa waandishi wa habari lina changamoto kubwa, kwa kuwa ni kikwazo kwa watu waaandishi wanaopenda ama kuhitaji



kuingia kwenye taaluma hiyo. Vigezo vya kutoa ithibati kwa waandishi wa habari havikuainishwa kwenye Sheria hii; hali inayotoa mwanya kwa Serikali kuweza kuwaengua bila kufuata utaratibu wowote waandishi wanaoikosoa kutoka kwenye tasnia hiyo, hasa kwa kuzingatia kwamba Waziri ndiye anayeteua wajumbe wa Bodi ya Ithibati ya Wanahabari.

Bodi ya Ithibati ya Wanahabari na Baraza Huru la Habari

- Bodi ya Ithibati ya Wanahabari (wajumbe saba wanaoteuliwa na Waziri) itatoa ithibati na vitambulisho kwa waandishi wa habari, itasimamia kanuni za maadili ya uandishi wa habari, na itasimamia na kuendeleza misingi bora ya maadili na nidhamu kwenye tasnia ya habari. Bodi inaweza kusimamisha au kuondoa wanahabari kutoka kwenye orodha ya wanahabari waliothibitishwa, kutoa adhabu ya faini kwa kukiuka kanuni, na kuweka ada na tozo mbalimbali katika zoezi la kutoa ithibati. [Vifungu 11-14]
- Kila mwandishi aliyethibitishwa atakuwa mwanachama wa Baraza, kwa mujibu wa Kifungu cha 24 cha Sheria hii. Kwa kushauriana na Bodi, Baraza litaweka kanuni za maadili kwa tasnia ya habari na litahimiza kufuatwa kwa misingi ya taaluma ya habari miongoni mwa wanahabari na vyombo vya habari. Baraza pia litafanya marejeo kuhusu utendaji wa vyombo vya habari, kushughulikia malalamiko mbalimbali yanayotokana na machapisho (magazeti), na



kuhimiza uwajibikaji kwenye tasnia ya habari.
[Kifungu cha 26]

Haki na Wajibu wa Waandishi kwa Habari

- Vyombo vya habari vya umma na vya binafsi vinaweza kukusanya habari kutoka vyanzo mbalimbali; kuchambua na kuhariri taarifa zilizokusanywa kwa kuzingatia maadili ya kitaaluma; na kuchapisha au kutangaza habari. Serikali ina udhibiti mkubwa kwa vyombo binafsi vya habari kwa kuvitaka kuchapisha na kutangaza kuhusu masuala yenye umuhimu kwa taifa. [Vifungu 6-7]
- Vyombo vya habari havitotoa au kusambaza taarifa: zitakazodhoofisha usalama wa nchi na upelelezi unaofanywa na vyombo vya sheria; zinazokwamisha taratibu za sheria na au kuhatarisha usalama wa maisha ya mtu yeyote; zinazolingilia faragha ya mtu yeyote; zinazozuia maslahi halali ya kibiashara ikiwemo haki miliki ya mmiliki, au zinazozuia au kusababisha madhara makubwa kwa Serikali katika kusimamia uchumi;
- Mtu yeyote atakayekwazwa na maudhui yaliyochapishwa kwenye gazeti au chapisho lolote anaweza kupeleka malalamiko yake kwenye kamati ya malalamiko ya Baraza ndani ya miezi mitatu tangu kuchapishwa kwa maudhui husika; Mamlaka ya rufaa dhidi ya fidia iliyotolewa yapo chini ya Mahakama Kuu. [Vifungu vya 20-29].



Athari: Mamlaka mbalimbali zinapewa madaraka kubwa katika kudhibiti maudhui na shughuli za kila siku za vyombo vya habari. Nguvu hizo, hasa kwa vyombo binafsi vya habari, zinaingilia uhuru wao wa uhariri na hivyo kuathiri kwa upana uhuru wa vyombo vya habari, kutoa maoni na kujieleza. Zaidi ya hapo, jamii inanyimwa haki yake ya kupata taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vya habari na maoni aina mbalimbali za maoni.

Mamlaka ya Polisi

- Jeshi la Polisi limepewa mamlaka pana ya kufanya upekuzi kwenye chombo cha habari na kukamata kifaa chochote kilichoanzishwa, kuwekwa, au kuendeshwa kwa kukiuka matakwa ya Sheria hii. [Kifungu cha 60]

Makosa chini ya Sheria Hii

- Kifungu cha 50 cha Sheria hii kinaeleza makosa na adhabu kwa kuchapisha habari kwa makusudi, uzembe, ya kutungwa na ya uongo, yenye nia ovu au ya kutungwa na ya uongo; au taarifa iliyokatazwa inayoweza kuhatarisha maslahi ya jamii, na hadhi, haki au uhuru wa watu wengine. Makosa mengine ni pamoja na kuendesha chombo cha habari bila ya kuwa na leseni, kufanya kazi ya uandishi wa habari bila ya kuthibitishwa na mamlaka husika, au kusambaza taarifa za uongo na zisizothibitishwa.
- Makosa yanayohusu kashfa pia yameainishwa kwenye Sheria hii. Hairuhusiwi kuchapisha ama kutangaza habari zenye kukashifu



isipokuwa tu iwapo habari hizo ni za kweli na zinabeba maslahi ya umma. Sheria inaeleza mazingira ambayo kuchapisha habari au taarifa za kashfa hakutochukuliwa kama ni kuvunja sheria, na ambayo mwanahabari husika hatoadhibiwa – hasa pale ambapo habari au taarifa husika inachapishwa na mamlaka za Serikali. Kuchapisha au kutangaza habari zinazohusu kashfa unaruhusiwa katika mazingira mbalimbali, hasa iwapo kutangaza au kuchapisha habari hizo kunafanywa kwa nia njema. [Vifungu vya 35-39].

Athari: Kufanya kashfa kuwa kosa la jinai kunakiuka haki ya uhuru wa kujieleza, na adhabu kama vile kifungo si kikwazo kinachokubalika katika kudhibiti uhuru wa kujieleza kwa lengo la kulinda haki na hadhi za watu wengine. Ujinaishaji huo wa kashfa unaweza kusababisha hali ya wanahabari kujidhibiti wenye katika kutekeleza majukumu yao. Kuna hatari ya kinga zinazopewa mamlaka za Serikali kuweza kuzima sauti zinazokosoa utendaji wa Serikali. Taarifa hizo muhimu hazilazimiki kuwa za kweli au kutolewa kwa nia njema. Hali hii inatoa hiyari na wigo mpana kwa Serikali na vyombo vyake kufanya maamuzi yasiyofuata taratibu na kuchapisha habari za uongo au zenye kashfa bila ya kuhofia kuwajibika, kupata madhara au adhabu yoyote.

Vitu Vilivyopigwa Marufuku

- Uingizaji, uchapishaji, uuzaji, usambazaji au uzalishaji wa vitu vilivyopigwa marufuku utachukuliwa kama makosa ya uchochezo kwa mujibu wa Kifungu cha 53. Chini ya



Kifungu cha 58 cha Sheria hii, Waziri ana hiari ya kuzuia uingizaji wa machapisho ambayo kwa maoni yake yatakwenda kinyume na maslahi ya umma. Vile vile, Waziri anaweza kuzuia uchapishaji wa maudhui yanayoathiri usalama wa nchi au wa jamii. [Kifungu cha 59].

Athari: Maamuzi yasiyofuata sheria yanayotegemea busara za Waziri yana changamoto zake. Hiari hiyo ya Waziri inaweza kutumia vibaya kwa kuzuia uingizwaji na uchapishaji wa bidhaa au machapisho yenye taarifa zisizoipendeza Serikali. Pia, Sheria hii haielezi kuhusu aina ya bidhaa au machapisho yanayoweza kuingia kwenye kundi la bidhaa zinazozuiwa, ili kuwawezesha wanahabari kujidhibiti kama inavyopasa kwa kutokiuka matakwa ya Sheria hii.

Vile vile, vitendo vya uchochezi vimetakwa kwa ujumla mno kwenye Sheria hii, hali inayoleta mashaka na kusumbua wanahabari katika kutafuta namna bora ya kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria. Pamoja na adhabu kali zilizowekwa, ni vigumu kwa mtu kugundua chapisho au taarifa yenye uchochezi au kufahamu mtu anayeamua kwamba taarifa fulani ni ya uchochezi. Mwandishi anaweza kuandika na kuchapisha taarifa inayodhaniwa kuwa ya uchochezi bila ya yeye kufahamu, au kuchapisha maudhui yasiyoipendeza Serikali na ambayo yanaweza kuonekana kuwa ni uchochezi baada ya kuchapishwa ama kutangazwa na chombo cha habari. Kuna hatari kwa vifungu vinavyoruhusu kunyang'anya vifaa vinavyohusishwa na uchapishaji wa taarifa za uchochezi kutumika kufanya vyombo vya habari



kushindwa kutekeleza majukumu yake, hasa iwapo vitashindwa kuendelea kutangaza au kuchapisha habari.

Sheria ya Kupata Habari, 2016

Lengo la msingi la Sheria hii ni kusaidia watu kupata taarifa; kueleza aina ya taarifa ambazo jamii ina haki ya kuzipata; na kusisitiza uwazi na uwajibikaji kwa vyombo au watu wenye taarifa.

Matumizi ya Sheria Hiyo

- Sheria hii inatumika kwa “vyombo au watu wenye taarifa” – ambao ni mamlaka za umma na mamlaka binafsi zilizosajiliwa chini ya sheria yoyote iliyoandikwa ambazo (i) hutumia fedha za umma au (ii) wanamiliki taarifa zenye maslahi muhimu kwa umma. [Kifungu cha 2(2)]
- Ni raia wa Tanzania pekee wenye haki ya kupata taarifa, haki inayoweza kudhibitiwa kwa mujibu wa sheria nyingine zilizoandikwa. [Kifungu cha 5]

Athari: Vyombo binafsi vya habari vinaweza kuhusika na Sheria hii kwa kuwa vinaweza kumiliki taarifa zenye maslahi kwa umma. Kutokana na hali hiyo, vyombo hivyo vinaweza kuhitajika kuweka wazi taarifa zilizo kwenye umiliki wao. Neno ‘maslahi ya umma’ halijafanuliwa na linaweza kusababisha kutolewa kwa taarifa za aina nyingi zikiwemo taarifa za utambulisho binafsi na zile zinazohusu masuala yasiyo ya umma.

Waandishi wa habari kutoka nje ya Tanzania hawawezi kupata taarifa kwa kuwa Sheria hii inawahusu raia wa Tanzania pekee.



*Maombi ya Kupata Taarifa na Wakati Taarifa
Zinapoweza Kutotolewa*

- Vifungu vya 10-17 vimeweka mchakato wa namna ya kuwasilisha maombi ya kupata taarifa.
- Vyombo au watu wenye taarifa wanaweza kuamua kutotoa taarifa iwapo taarifa husika haistahili kutolewa, na iwapo kutolewa kwa taarifa husika hakujathibitishwa kuwa ni kwa maslahi ya umma. Mazingira hayo hujumuisha iwapo taarifa husika zitahujumu au zitadhoofisha ulinzi, usalama wa nchi, na uhusiano wa kimataifa; kuzuia au kusababisha madhara makubwa kwa Serikali na uchumi; na kuathiri kumbukumbu za Baraza la Mawaziri na kamati zake mbalimbali. Adhabu zinatolewa kwa kuweka wazi taarifa zisizostahili. [Kifungu cha 6]
- Rufaa dhidi ya chombo au mtu mwenye taarifa huweza kuwasilishwa ndani ya siku 30 baada ya kutolewa kwa uamuzi au majibu husika kutokana na taarifa iliyoombwa.
- Mamlaka ya rufaa ya ngazi ya juu yamo mikononi mwa Waziri, isipokuwa iwapo chombo au mtu mwenye taarifa husika atakuwa chini ya Waziri, hali itakayolazimu mkata rufaa kupeleka maombi ya marejeo kwenye Mahakama Kuu. [Kifungu cha 19]

Athari: Vipengele vya sheria nyingine vinaweza kuathiri kutolewa ama kuwekwa wazi kwa taarifa kwa mujibu wa



matakwa chini ya Sheria hii. Sheria hii inatoa upekee au msamaha mpana na wa aina nyingi kuhusiana na taarifa inayoweza kufichwa au kutotolewa, inatoa wigo mpana wa matumizi ya busara binafsi kwa vyombo au watu wenye taarifa kuamua aina ya taarifa yenye maslahi ama isiyo na maslahi kwa umma, na ina lugha butu isiyofafanua ipasavyo inayoweza kusababisha kuzuiwa, kufichwa ama kutowekwa wazi kwa taarifa taarifa na nyaraka za aina nyingi. Waandishi wa habari wanaweza kupata ugumu katika kubashiri kwa uhakika aina ya taarifa wanazoweza kuzitafuta, kuzipata au kuziweka wazi.

Kuweka wazi taarifa isiyostahili hupelekea adhabu kali za kihalifu, bila ya kujali iwapo taarifa husika ilitolewa kwa nia njema au la.

Makosa Chini ya Sheria Hii

- Sheria hii inaorodhesha makosa anuai, yakiwemo kupotosha taarifa (linalobeba adhabu ya kifungu cha kati ya miaka miwili hadi mitano gerezani – Kifungu cha 18); kubadili, kuzuia, kufuta, kuharibu au kuficha taarifa kwa nia ya kuzuia taarifa hizo kuwekwa wazi (Kifungu cha 22).
- Mtu yeyote mwenye taarifa, kutokana na ajira au majukumu yake ya kikazi, atatoa taarifa kwa nia njema kuhusu uvunjifu wa sheria (kama vile taarifa zinazohusisha uhalifu, kushindwa kutekeleza amri halali kisheria, kutofuata sheria, ufisadi, matumizi mabaya ya mamlaka kuhusiana na chombo au mtu mwenye taarifa) au kuweka wazi taarifa



zinazoweza kuhatarisha afya ya jamii usalama au mazingira, hatowajibishwa kwa mujibu wa taratibu zozote za kiutawala, kisheria au ajira. [Kifungu cha 23]

- Maafisa walioajiriwa au wanaohudumu kwenye chombo chochote chenye taarifa hawatowajibishwa kwa utaratibu wa sheria za madai au jinai kwa vitendo walivyofanya au walivyoacha kufanya wakiwa na nia njema. [Kifungu cha 24]

Athari: Watu wowote wasioridhika au wanaokwazwa na sheria ya kupata taarifa, kwa ujumla, hawawezi kupeleka mashauri yoyote mahakamani kuomba mapitio ya uamuzi uliotolewa unaowanyima haki ya kupata taarifa. Kukosekana kwa mchakato huru wa kisheria au kimahakama katika kusikiliza na kuamua mashauri hayo kunaashiria kwamba matumizi ya kiimla na yasiyofaa ya kisheria, yakiwemo yale yanayoathiri maandishi wa habari katika kutekeleza majukumu yao, hayatoshughulikiwa ipasavyo.

Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, 2010

Sheria inahusu:

- udhibiti wa watoa huduma za mawasiliano ya kielektroniki na posta;
- usajili wa namba (laini) za simu;
- utoaji wa vibali (leseni) kwa shughuli za mawasiliano na posta;
- udhibiti wa masuala ya leseni, mawakala na



wateja, maudhui, ushindani, na utendaji;

- makosa yanayohusiana na mawasiliano ya kielektroniki na posta.

Vipengele vinavyohusu na athari za Sheria hii kwa vyombo vya habari ni pamoja na:

Leseni

Vifungu vya 4-22 vinaeleza kuhusu chombo chenya mamlaka ya kutoa leseni, yaani Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano Tanzania (Mamlaka ya Mawasiliano / TCRA), aina ya leseni zitakazotolewa, mchakato wa kufuata, masharti ya kuhuisha, kusimamisha na sitisha leseni.

Masuala Yanayohusu Mawasiliano kwa Njia ya Posta

- Vifungu vya 36-40 vinahusu mawasiliano ya posta na utoaji wa leseni kwa ajili ya mawasiliano ya posta.
- Kifungu cha 42 kinalinda faragha ya mawasiliano na kinatoa orodha na misamaha (exceptions) kwa sheria husika. Masuala yanayohusu kuwajibika kwa kupotea, kuweka mahali pasipostahili, kupeleka au kushindwa kuhakikisha usalama na uhalisia wa bidhaa au vifurushi vilivyotumwa kwa njia ya posta, na fidia, yanatolewa ufafanuzi katika Kifungu cha 43.
- Vifungu vya 46 na 52 vinaeleza kuhusu mawasiliano yaliyopigwa marufuku au bidhaa ama vifurushi ambavyo mtu mwenye leseni ya kutoa huduma za posta anaweza kuvikataa.



- Kifungu cha 53 kinazuia kusambaza kwa njia ya posta bidhaa au kitu chochote kinachokiuka maadili ya jamii: Vitu hivyo ni pamoja na: machapisho, michoro, picha, bidhaa za uchongaji, kitabu au kadi na kitu kingine chochote chenye matusi au kinachokiuka maadili ya jamii; kitu chochote kinachoweza kutumwa kwa njia ya posta chenye kasha lenye maneno, alama, au ubunifu unaoashiria ukiukwaji wa maadili, matusi, uchochezi, kashfa, vitisho, au muhusika anayeashiria kuvuruga amani.

Mawasiliano kwa Njia ya Redio

- Vifungu vya 71-72 vinaipa Mamlaka ya Mawasiliano nguvu za kusimamia na kudhibiti masafa yote ya mawasiliano ya redio wa kutoa leseni, ikiwemo kutoa masafa ya matangazo, kubadili masafa ya matangazo, kusimamisha, kusitisha au kufanya mabadiliko mengine ya masafa na usambazaji wa matangazo. Mamlaka ya Mawasiliano huweka madaraja mbalimbali kwa vituo vya redio, huelekeza aina ya huduma zitakazotolewa na vituo vya redio, na hutoa masafa ya utangazaji na muda kituo husika kinaweza kurusha matangazo. Vipengele hivyo vinaeleza utaratibu wa kufuatwa pindi Mamlaka ya Mawasiliano inapochunguza au kuhoji kuhusu matumizi ya masafa yaliyotolewa kwa kituo au vituo vya redio.
- Vifungu vya 85-102 vinaeleza kuhusu usajili wa namba za simu na simu za mkononi, usiri



wa taarifa na kuzimwa kwa simu zilizoibwa, zilizopotea, au zilizoharibika.

Athari: Ulazima wa kusajili namba za simu unaweza kuleta changamoto kwa waandishi wa habari kulinda utambulisho wa vyanzo vyao vya taarifa na kuhakikisha usiri wa taarifa wanazozipata kutoka kwa vyanzo hivyo.

Masharti yanayowataka waandishi wa habari kutangaza kipindi kinachokinzana na kile walichotangaza awali yamewekwa pasipo kuzingatia madhara na uhalisia uliopo kiutendaji. Kutekeleza masharti hayo kunaweza kusababisha mzigo mzito kwa vyombo vya habari kutokana na wingi wa matakwa yanayofanana kutoka pande mbalimbali zitakazodai kukwazwa na kipindi au matangazo fulani. Hali hiyo itaathiri uhuru wa uhariri kwenye vyombo vya habari, pamoja na utayari wa vyombo vya habari kutangaza kuhusu masuala tete yanayobeba maslahi ya umma.

Masuala ya Maudhui

- Kifungu cha 103-4 kinaeleza kuhusu kanuni za maadili zenye nguvu ya kisheria, na zinapiga marufuku kutangaza maudhui ya uongo, yenye matusi, yenye vitisho, na yanayokiuka maadili ya jamii au yanayokwaza kwa ujumla. Kanuni hizo za maadili zinalenga kulinda watoto; kukataza au kupunguza uhalifu; kutangaza habari zinazoeleweka, sahihi, na zisizoegemea upande wowote; kutangaza maudhui ya kidini kwa usawa na kuonesha kujali; na kulinda maslahi ya umma dhidi ya maudhui yasiyofaa na yanayoweza kuleta madhara.



- Mamlaka ya Mawasiliano inaweza kuweka kanuni kwa lengo la kuhakikisha kwamba vituo vyenye leseni ya utangazaji vinatangaza mara kwa mara habari kuhusu matukio yanayotokea kwa usahihi, na kwa nkwa kuhakikisha usawa na haki. [Kifungu cha 106]
- Kifungu cha 107 kinaeleza kuhusu udhibiti wa maudhui huru, yanayoendana na yanayoakisi uhalisia wa Tanzania, na kinazuia urushaji wa vipindivyenyemaudhuiyasiyoendana au kuwa na umuhimu kwa maendeleo na mazingira ya kijamii nchini Tanzania. Kifungu hicho pia kinaeleza kiwango ambacho maudhui huru, na yanayoendana na kuakisi mazingira ya Tanzania yatajumuishwa; vilevile kinaeleza muda wa siku na wiki ambapo maudhui hayo yatarushwa hewani.
- Sheria haikatazi kurusha matangazo yenye maudhui ya kisiasa. Hata hivyo, Waziri anaweza kudhibiti matangazo hayo kwa namna inayoendana na malengo, maelekezo na kanuni, haki za msingi na wajibu kama ilivyoainishwa kwenye Katiba. [Kifungu cha 112]
- Mmiliki wa leseni ya huduma za maudhui atalazimika kurusha kipindi chenye maudhui kinzani na yale aliyorusha awali kwa kuzingatia malalamiko yatakayotolewa na mtu atakayedai kwamba taarifa zilizorushwa kwenye kipindi cha awali hazikuwa sahihi,



isipokuwa iwapo mtu au taasisi iliyohusishwa na taarifa hizo zisizo sahihi haitokuwa na maslahi ya moja kwa moja kwenye kurusha kipindi hicho chenye maudhui kinzani, au kwamba kipindi hicho cha maudhui kinzani hakitohitajika kuwa na urefu unaoweza kuathiri au kurekebisha kosa lililofanyika. [Kifungu cha 113]

Athari: Mamlaka ya Mawasiliano imepewa madaraka makubwa mno katika kudhibiti maudhui kwa kutumia lugha butu na maneno kama vile “ya matusi”, inayokiuka maadili”, “ya vitisho”, na “inayokwaza” yasiyofafanua masuala muhimu kwa ufasaha. Itakuwa vigumu kwa waandishi wa habari na vyombo vya habari kufahamu au kutarajia aina ya maudhui yanayokwenda kinyume na Sheria hii. Kwa kufanya hivyo, Serikali inakuwa na nguvu isiyohojika kuweza kupiga marufuku maudhui yasiyoipendeza wakati wowote inapotaka kufanya hivyo. Waziri amepewa mamlaka makubwa sana ya kutumia busara zake kuelekeza namna namna ambavyo kutangaza vipindi vya maudhui ya kisiasa, hali inayoathiri uhuru wa sera huru ya uhariri kwenye vyombo vya habari.

Mamlaka ya Polisi

- Maafisa wa polisi au wafanyakazi walioruhusiwa na Mamlaka ya Mawasiliano wanaweza kuingia, kukagua, na kutwaa vifaa vya mawasiliano kutoka jengo au mahali popote pindi kunapokuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba Sheria hii au kanuni zake zimekiukwa. [Kifungu cha 163]



Athari: Vyombo vya habari vinaweza kufanyiwa upekuzi, au vitendea kazi vyao kutwaliwa na mamlaka za usimamizi wa sheria bila ya kuwapo kwa hati ya upekuzi au mchakato mwingine wowote wa kisheria au wa utaratibu wa kimahakama. Hali hii inaathiri utendaji wa vyombo vya habari na kusababisha vyanzo vya taarifa kushindwa kuviamini vyombo vya habari, na hivyo kutovipatia vyombo hivyo taarifa muhimu.

Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Habari za Mtandaoni), 2018

Vipengele muhimu na athari zake kwa vyombo vya habari ni pamoja na:

Masharti ya Kusajili na Wajibu kwa Uchapishaji wa Maudhui

- Kanuni ya 4 – Mamlaka ya Mawasiliano imepewa mamlaka ya kusajili blogu, majukwaa ya mtandaoni (online forums), redio na televisheni (runinga) zinazorusha matangazo kwa njia ya mtandao wa intaneti (redio za mtandaoni); kuchukua hatua kwa kukiuka kanuni hizo; kuendesha kampeni za kuongeza mwamko wa jamii kuhusu kanuni hizo za matumizi salama ya maudhui ya mtandaoni.

Athari: Masharti ya usajili wa lazima yanahusu blogu na majukwaa ya mtandaoni, na pia kimsingi yanahusu waandishi wa habari na watumiaji wengine wa mitandao ya kijamii. Uwezo wa TCRA kukataa kusajili chombo chochote cha habari mtandaoni unamaanisha kwamba Mamlaka ya Mawasiliano ina uwezo wa kuchagua maoni au sauti ya mtu au chombo inayotakiwa kusikika na ile isiyotakiwa



kusikika. Hivyo, Mamlaka ya Mawasiliano inaweza kuamua kunyamazisha waandishi wa habari wanaofuatilia utendaji wa Serikali na vyombo vyake kwa niaba ya jamii na wakosoaji wengine.


Utoaji wa Leseni za Maudhui, Wajibu kwa Uchapishaji wa maudhui, na Kanuni kuhusu Maudhui Yaliyokatazwa

- Kanuni za 14-15 – Watoa huduma za maudhui wana wajibu wa kuomba leseni, na Mamlaka ya Mawasiliano inaweza kusitisha leseni hizo pindi kunapotokea ukiukwaji wa vigezo na masharti yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.
- Kanuni ya 10 – Watumiaji wa mitandao ya jamii watawajibika kwa taarifa wanazochapisha mtandaoni.
- Kanuni ya 5 – Watoa huduma ya maudhui mtandaoni wana wajibu wa kuhakikisha kwamba maudhui yanayochapishwa ni salama na yanafuata sheria zilizopo. Wana wajibu wa kuchuja na kuondoa maudhui yaliyokatazwa; kuchukua hatua za kurekebisha maudhui yanayobishaniwa au yaliyokatazwa; na kuhakikisha kwamba maudhui yaliyokatazwa yanaondolewa ndani ya saa kumi na mbili tangu kutolewa kwa taarifa kuhusu uwapo wake kwenye mtandao husika.
- Kanuni ya 7 – Watoa huduma waliopewa leseni za kuendesha vituo vya redio na runinga vinavyorusha matangazo mtandaoni wana wajibu wa kufuata kanuni za huduma hiyo,



maadili ya uandishi wa habari, na masharti ya kutangaza maudhui ya ndani yanayoakisi uhalisia na maslahi ya nchi (local content).

- Kanuni ya 6 – Watoa huduma walioruhusiwa (wanaomiliki leseni inayohusu kurusha maudhui au kuwezesha uwekaji wa maudhui mtandaoni) wana wajibu wa kuhakikisha kwamba watumiaji wa huduma husika wanafuata kanuni, ikiwemo kumuarifu mtumiaji husika kuondoa maudhui yaliyopigwa marufuku. Kushindwa kufanya hivyo kutapelekea mtoa huduma huyo kusimamisha au kusitisha akaunti ya mtumiaji wa huduma husika.
- Kanuni ya 12 – inaeleza kuhusu maudhui yaliyopigwa marufuku mtandaoni ikiwemo matusi, kauli za chuki, maudhui ya ngono, maudhui yanayosababisha kero, yanayotishia usalama au kusababisha ubaya, yanayochochea uhalifu au kusababisha uvunjifu wa amani, maudhui yanayoweza kusababisha hatari kwa afya ya jamii na amani ya nchi kama vile kuleta usumbufu kwenye sehemu fulani ya nchi; maudhui yanayotumia lugha isiyofaa kama vile lugha ya kebehi na matusi yanayolenga kuumiza au kuudhi mtu au kiundi fulani cha watu, na habari zenye maudhui ya uongo zinazoweza kupotosha jamii isipokuwa iwapo maudhui hayo yatatajwa kuwa ni kejeli, ubishi, au hadithi au jambo lisilo na uhalisia.

- 
- Kanuni hizo zinaeleza mchakato utakaofuatwa na mtu yeyote atakayetaka kuwasilisha malalamiko kwa mtoa huduma za maudhui mtandaoni kuhusiana na maudhui yaliyokatazwa au kupigwa marufuku.

Athari: Maneno “mtoa huduma za maudhui mtandaoni” hayakufafanuliwa, na hivyo yanaweza kujumuisha redio, runinga (televisheni), mitandao ya kijamii, blogu na huduma nyingine za habari za kielektroniki. Mtu yeyote anaweza kupeleka malalamiko dhidi ya mtoa huduma za maudhui mtandaoni kuhusiana na maudhui yaliyokatazwa. Watoa huduma za maudhui mtandaoni, watumiaji wa mitandao ya kijamii, na waandishi wa habari wanalazimika kuondoa maudhui yaliyokatazwa au yanayodhaniwa kutofaa, au kushughulikia malalamiko kutoka Mamlaka ya Mawasiliano au mtu yeyote ndani ya saa kumi na mbili. Utekelezaji wa masharti hayo unasababisha kutokuwapo kwa fursa ya kuhoji uhalali wa malalamiko husika na mchakato unaoweza kutumika kudhibiti (censor) maudhui yanayochapishwa ama kurushwa mtandaoni. Kushindwa au kukataa kushughulikia malalamiko husika kutapeleka kuhusishwa ama kushughulikiwa kwa uhalifu kwa mujibu wa sheria. Waandishi wa habari wanaochapisha au kurusha maudhui yaliyokatazwa bila ya kujli malalamiko yaliyopo wanaweza kukabiliwa na adhabu kali, ikiwemo faini na kifungo gerezani.

Matumizi ya maneno kama vile “matusi”, “yanayokiuka maadili ya jamii”, “lugha mbaya”, na “uongo” yenye maana butu na isiyo ya moja kwa moja husababisha kuibuliwa kwa fasili za aina mbalimbali kutokana na kutokuwapo kwa ufafanuzi wa wazi wa kisheria. Mamlaka za Serikali



zinaweza kutumia mwanya huo kutumia busara zake za kimaamuzi kushughulikia watu au taasisi kwa kutumia utaratibu wa sheria za uhalifu dhidi ya watu, pamoja na waandishi wa habari, wanaochapisha au kutangaza taarifa zinazoikosa serikali na mamlaka zake.

Kuna utata katika makundi ya maudhui yaliyopigwa, mapana mno, na yanaweza kusababisha hatari ya kuzuia waandishi wa habari kuchapisha au kurusha matangazo yenye habari na taarifa muhimu. Kwa mfano, habari kuhusu vurugu, uhalifu wa kutumia nguvu, au kampeni zinazoeleza madhara ya ukatili wa majumbani, na biashara haramu ya uuzaji wa binadamu (human trafficking) zinaweza kuchukuliwa kama ukiukwaji wa Kanuni hizi.

Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano, 2003

Sheria hii inaunda Malaka ya Udhhibiti wa Mawasiliano (TCRA, kwa ufupisho kwa lugha ya Kingereza) kama chombo cha udhibiti wa mawasiliano ya simu, utangazaji, huduma za posta, na kinachotoa masafa ya urushaji wa matangazo na mawasiliano kwa redio, teknolojia za kielektroniki na huduma nyingine za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). The

Vipengele muhimu na athari zake kwa vyombo vya habari vinajumuisha:

Kazi na Majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano na Bodi Yake ya Wakurugenzi

- Kazi na majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano yameelezwa kwenye Vifungu vya 5 na 6 na zinajumuisha kutoa, kuhuisha,



na kusitisha leseni, na kuweka vigezo vitakavyoongoza utoaji wa huduma na bidhaa zinazohusu mawasiliano.

- Kuundwa kwa bodi na kazi zake kueainishwa kwenye Vifungu vya 7-12. Bodi hiyo itahusika na uendeshaji wa Mamlaka ya Mawasiliano na itaundwa na watu saba watakaoteuliwa na Rais na Waziri mwenye dhamana ya Mawasiliano (isipokuwa kwa masuala yanayohusu udhibiti wa kanuni na maudhui yanayohusu na utangazaji).
- Kifungu cha 26 kinaunda Kamati ya Maudhui na kueleza kuhusu uanachama wake. Waziri anateua Kamati hiyo Kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Waziri huteua Kamati hiyo. Kazi za kamati ni pamoja na kumshauri Waziri mwenye dhamana kuhusu sera ya utangazaji, kusimamia na kudhibiti maudhui katika sekta ya utangazaji, kupokea na kushughulikia malalamiko kutoka kwa vyombo vya utangazaji na hadhira (watumiaji wa vyombo hivyo) kuhusu ukiukwaji wa maadili. [Kifungu cha 27]
- Malalamiko dhidi ya kutoridhishwa na uamuzi uliotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano yanaweza kuwasilishwa kwa Kamati ya Marejeo, iliyoundwa chini ya Kifungu cha 33 cha Sheria hii. Rufaa za ngazi za juu dhidi ya uamuzi wa Mamlaka ya Mawasiliano au uamuzi wowote kuhusiana na malengo ya



Sheria hii zinaweza kuwasilishwa Baraza la Ushindani wa Haki. [Kifungu cha 36]

Athari: Hali ya Mamlaka ya Mawasiliano kukosa uhuru, hasa katika kuteua wanachama wake, inaibua wasiwasikwamba Rais na Waziri, ambazo ni mamlaka zinazofanya uteuzi huo, wanaweza kuwadhibiti wateuliwa hao kwenye kutekeleza majukumu yao, hasa katika mwelekeo wa sera zinazotekelezwa na Mamlaka ya Mawasiliano.

Mamlaka [Powers] ya Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA)

- Mamlaka ya Mawasiliano inaweza kutoa amri ya utii pindi inapojiridhisha kwamba mtu au chombo kimetenda kosa au kinaelekea kutenda kosa chini ya Sheria hii au sheria yoyote inayohusu sekta ya mawasiliano (sheria inayohusu sekta ya vyombo vya habari au huduma za habari). Amri hiyo inaweza kumtaka mtu kusitisha kitendo kinachovunja Sheria au kuchukua hatua zitakazohakikisha kuendana na kufuata misingi na matakwa ya Sheria hii na sheria nyingine za sekta yay a habari. Amri ya utii itatekelezwa na kuwa na nguvu sawa na amriiliyotolewa na Mahakama Kuu. [Kifungu cha 45]

Athari: Mamlaka ya Mawasiliano imepewa mamlaka makubwa ya kusimamia utekelezaji wa sheria katika udhibiti wa uanzishwaji wa vyombo vya habari na vyombo vingine vya mawasiliano, uendeshaji wake, na maudhui ya taarifa zinazochapishwa au zinazorushwa kwenye matangazo ya redio, runinga na njia nyingine.



Sheria inayoshughulikia vyombo vya habari ina mapungufu anuai, ambayo yanaweza kutumiwa vibaya na Mamlaka ya Mawasiliano. Mapungufu hayo ni pamoja na:

- masharti yanayolazimu kupata leseni na kujisajili;
- maneno yenye maana pana na butu (zisizoeleza undani wa kitu audhana) katika kutaja vitendo na maudhui yaliyokatazwa au kupigwa marufuku;
- uhusika na uwajibika wa kati katika kuondoa maudhui na kutoa taarifa kuhusu uwapo wa maudhui yaliyopigwa marufuku, ujinaishaji wa kashfa, pamoja na uchochezi;
- kutokuwapo kwa mchakato wa kisheria au utaratibu wa kimahakama kwa vitendo na kanuni zinazoingilia haki na uhuru wa mtu au kitu (intrusive) vikiwemo vitendo vya upekuzi na kutwaliwa kwa vifaa mbalimbali.

Kanuni za Huduma za Utangazaji (Maudhui), 2005

Vipengele Muhimu

- kanuni ya 5 – vyombo vyote vyenye leseni ya kutoa huduma ya utangazaji vina wajibu wa kuhakikisha kwamba vipindi vinavyorushwa na namna ya utangazaji wake:
 - vinaendeleza uhuru wa nchi kujitawala, maslahi ya nchi, usalama wa nchi, na maslahi ya kiuchumi ya nchi ya Tanzania;



- kutangaza sifa za Tanzania na mtazamo wa taifa kuhusu masuala mbalimbali;
 - kufuata na kusimamia maadili;
 - kuendeleza na kusimamia maadili ya jamii;
 - kuepuka kufanya vitendo vinavyoingilia faragha na maisha binafsi ya watu;
 - kutokuharibu heshima ya watu;
 - kulinda watoto dhidi ya vishawishi vibaya;
 - kutokuchochea au kueneza chuki dhidi ya, au kutweza mtu au kikundi chochote cha watu kwa misingi ya ukabila, rangi, jinsia, dini au ulemavu.
- Wamiliki wa leseni za utangazaji wana wajibu wa kutangaza habari kwa muda usiopungua saa moja na nusu kila siku. Kanuni ya 6 inafafanua aina ya habari – za kieneo, kikanda, kitaifa, na kimataifa – na kuzingatia usahihi wa taarifa, haki, zenye uyakinifu, na zisizoegemea upande wowote.
 - Kanuni ya 9 – kulinda faragha. Mmiliki wa leseni ya utangazaji haruhusiwi kutumia masuala binafsi ya mtu isipokuwa tu iwapo kuna sababu za msingi zinazohusu maslahi ya umma. Utambulisho wa wahanga wa matukio ya ubakaji na madhila mengine ya kingono hautowekwa wazi isipokuwa kwa ridhaa ya maandishi kutoka kwa wahanga hao.



Utambulisho wa watoto wahanga wa matukio hayo hautawekwa wazi kabisa.

- Kanuni ya 15 – Kanuni hii inakataza matumizi ya lugha isiyo rasmi bila ya kupata ruhusa maalum, na inasisitiza kuweka umakini mkubwa katika kuhakikisha kwamba lugha hiyo haipotoshi au kusababisha taharuki, wasiwasi, huzuni na rabsha pasipo sababu za msingi. Umakini wa hali ya juu unahitajika katika kuzingatia tofauti za kidini na kitamaduni na ili kuepuka kukufuru.
- Kanuni ya 16 inaeleza namna ya kuandika ama kutangaza habari zinazohusu ngono, na Kanuni ya 18 inaeleza kuhusu namna kuandika ama kutangaza habari zinazohusu vurugu. Kanuni ya 20 inalenga kuzuia ubaguzi unaotokana na imani potofu na uliokatazwa kwa namna nyingi, ukiwemo ubaguzi kwa misingi ya jinsia na ulemavu.
- Kanuni hizo zimebeba vikwazo mbalimbali vyenye mashiko kisheria dhidi ya haki ya uhuru wa kujieleza na haki mbalimbali za vyombo vya habari kwa lengo la kupunguza ushawishi wa makampuni na wadhamini, kuhakikisha uwiano na usawa katika kutangaza habari zinazohusiana na uchaguzi, na kusisitiza haki katika kutangaza habari. [Vifungu vya 7, 8, na 11]



Athari

- Masharti ya lazima ya kufuatwa kwenye sekta ya utangazaji yanakiuka dhana ya uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa uhariri, hasa kwa vyombo vya habari binafsi ambavyo visingependa, kwa mfano, kutangaza habari au matukio yanayotokea kwa wakati husika mara kwa mara.
- Kanuni hizo pia zimebeba mifano mingi ya matumizi ya lugha butu (isiyofafanua dhana husika kwa kina), hali inayoweza kusababisha kutolewa kwa ufafanuzi au fasili potofu. Vile vile, kanuni hizo hazitoi mwongozo unaoeleweka kwa vyombo vya habari na waandishi wa habari utakaowawezesha kujitathmini kiutendaji kama inavyopaswa. Kwa mfano, masharti yanayotaka kutangaza vipindi vinavyoendeleza dhana za uhuru wa nchi kujitawala, umoja, maslahi ya taifa, na usalama wa nchi, au masharti ya kuzingatia maadili ya jamii kimsingi hayana vigezo vya uyakunifu (objectivity) vinavyoweza kukubaliwa na kila mdau. Kwa hali hiyo, watendaji mbalimbali kwenye vyombo vya habari wanaweza kujiikuta wakijidhibiti wenyewe katika kutekeleza majukumu yao kutokana na kujawa na wasiwasi wa kuogopa kufungiwa.



SHERIA ZINAZOZUIA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI

Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015

Sheria hii inahusu makosa yanayohusiana na mifumo ya kompyuta na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA); na uchunguzi, ukusanyaji na matumizi ya ushahidi wa kielektroniki na unaohusiana na hayo.

Vipengele muhimu na athari zake kwa tasnia ya habari ni pamoja na:

Makosa na Adhabu

- Vifungu vya 4-29 vinaeleza kuhusu makosa na adhabu kuhusiana na mifumo ya kompyuta [kifaa au mchanganyiko wa vifaa, ikijumuisha mtandao, vifaa vya kuingizia na vya kutolea na ambavyo vinaweza kutumika pamoja na majalada yaliyo na programu za kompyuta, maelezo ya kielektroniki, data za kuingizia na data za kutolea zinazotunza data za hesabu zilizo na mantiki na udhhibiti wa utolewaji wa mawasiliano na majukumu mengine] na teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Makosa yanajumuisha kupata, kuingilia, kumiliki, kukwepa mawasiliano isivyo halali, na kuingilia mfumo wa kompyuta au taarifa (data).
- Vifungu vya 13 na 14 kwa ujumla vinazuia uchapishaji wa picha za ngono zinazohusisha watoto wadogo (ponografia).
- Kifungu cha 16 kinazuia uchapishaji wa



taarifa au data ya uongo, ya kilaughai, yenye kupotosha au isiyo sahihi kwa nia ya kukashifu, kutishia, kutukana, au kupotosha jamii kwa namna yoyote.

- Kifungu cha 20 kinaainisha makosa kwa kusambaza, au kurusha au kusambaza tena taarifa zinazotumwa bila ridhaa, au kughushi taarifa za utambulisho na kuzituma bila ridhaa, yaani taarifa au data za kielektroniki ambazo hajaikuombwa na mpokeaji.
- Kifungu cha 23 kinazuia kutumia mawasiliano ya kielektroniki kwa lengo la kulazimisha, kutishakurubuni, kunyanyasa, au kusababisha madhara ya kiakili kwa mpokeaji.

Athari: Vipengele vya sheria vinavyoainisha au kufafanua makosa vinaweza kutumika kuadhibu waandishi wa habari, wafichua uhalifu, na wafuatiliaji wa utendaji wa vyombo au taasisi mbalimbali. Vipengele hivi vinaweka aina fulani ya adhabu hata kama hakukuwa na nia ya kutenda jinai au madhara makubwa kwa mwathirika. Hivyo, matumizi halali na yasiyokuwa na nia ovu ya data au taarifa kwenye mfumo wa kompyuta yamejinaishwa. Watu binafsi kama vile waandishi wa habari, ambazo kazi zao huhusisha kubadilishana taarifa kama sehemu ya majukumu yao, wanaweza kukutwa na makosa kwa vitendo walivyofanya bila ya kuwa na nia ovu pindi wanapokea au kusambaza taarifa au data za mfumo wa kompyuta huku wakiamini kwamba wanaruhusiwa kufanya hivyo bila ya kufahamu muktadha wa namna taarifa hizo zilivyosambazwa au kupatikana.



Waandishi wa habari wanaochapisha habari za kosa watu binafsi au mamlaka mbalimbali wanaweza kuchukuliwa kana kwamba 'wamewatukana' au wametoa taarifa 'za uongo' 'za kupotosha' au 'zisizo sahihi'. Ufafanuzi wa aina hii ni butu, hautoshelezi na haumwezeshi mtu kutambua waziwazi masuala yaliyojinaishwa. Hali hii inaweza kusababisha kuwatega waandishi wa habari pasipo kufuata sheria, au waandishi kujidhibiti wenyewe wanapoteketeza majukumu yao kutokana na woga wa kushughulikiwa na vyombo vya sheria. Imani ya umma kwa waandishi wa habari na dhima yao kama wafuatiliaji wa utendaji wa shughuli mbalimbali kwenye jamii huhujumiwa kwa kuitwa waongo au wasambazaji wa taarifa 'habari potofu'.

Mamlaka ya Polisi

- Kifungu cha 31 kinawapa mamlaka polisi au watekelezaji wa sheria wanaosimamia kitu cha polisi au wenye cheo kinachofanana kutoa amri inayoruhusu kuingia, kupekua, au kutwaa vifaa na mifumo ya kompyuta, na kutwaa data au taarifa zilizohifadhiwa kwenye kompyuta, iwapo watajiridhisha kwamba kuna sababu za msingi kuamini kwamba mfumo huo wa kompyuta unaweza kutumika kama sehemu ya ushahidi kwa husika au ni matokeo ya kosa hilo.
- Kwa mujibu wa Kifungu cha 32, afisa wa utekelezaji sheria anaweza kumtaka mtu anayemiliki data au taarifa zinazohitajika katika uchunguzi wa makosa au uendeshaji wa mashauri ya jinai kuweka wazi taarifa hizo.



- Kifungu cha 34 kinawapa mamlaka maafisa wa polisi kumtaka mtu anayemiliki taarifa au data zinazohitajika kwa ajili ya uchunguzi kuweka wazi, kukusanya, au kurekodi mwenendo wa taarifa au data za mawasiliano ya aina fulani, au kumruhusu na kumsaidia afisa wa utekelezaji sheria kukusanya au kurekodi taarifa hizo. Taarifa au data hizo ni zile zinazoonesha chanzo, mwisho, njia, na muda wa mawasiliano husika.
- Chini ya Kifungu cha 35, polisi wanaweza kutoa amri ya kukusanya, kurekodi, kuruhusu au kusaidia mamlaka sahihi kukusanya au kurekodi data au taarifa yenye maudhui yanayoainisha mawasiliano fulani ikiwemo matumizi ya njia za kiufundi, kitaalam au kiteknolojia. Kifungu cha 37 kinaruhusu polisi kutumia kifaa cha uchunguzi katika kukusanya data au taarifa kwa ruhusa ya mahakama, mwanzoni kwa muda wa siku kumi na nne, kipindi kinachoweza kuongezwa kwa ridhaa ya mahakama kwa kadiri itakavyoona inafaa kufanya hivyo. Utaratibu wa kusikiliza maombi ya namna hiyo utahusisha upande wa mwombaji pekee na hauruhusu kuhudhuriwa na umma au pande zozote zisizohusika.

Athari: Sheria hii inaruhusu kuingia, kupekua na kutwaa taarifa, data na vifaa. Maafisa wa utekelezaji sheria wanaweza pia kutoa amri inayolazimu kuwekwa wazi au kutolewa kwa taarifa. Katika mazingira mengi, vitendo hivyo vimeruhusiwa bila ya kusimamiwa na sheria au



mchakato wa kimahakama. Pindi utaratibu wa kisheria unapoainishwa, mchakato wa kusikiliza maombi husika huhudhuriwa na mwombaji pekee, hauruhusu umma kuhudhuria, na waathirika hawapati nafasi ya kusikilizwa. Waandishi wa habari na watendaji wengine wanaweza kumiliki au kuweza kupata taarifa inayoweza kuwa na maslahi au kuvuta umakini wa maafisa wa utekelezaji wa sheria. Hali ya kutokuwapo kwa utaratibu sahihi na wa wazi wa kisheria au mchakato wa kimahakama inaondoa kinga muhimu zinazoruhusu waandishi wa habari kutumia haki yao ya uhuru wa vya habari, ikiwamo kulinda vyanzo vyao vya taarifa.

Wajibu wa Watoa Huduma

- Kifungucha³⁹ kinazuiawatoa huduma kufuatilia data au taarifa anayoisambaza au kuihifadhi, au kutafuta taarifa za viashiria vya shughuli zinazohusisha uvunjaji wa sheria. Waziri (mwenye dhamana ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) anaweza kuwataka watoa huduma kuziarifu mamlaka kuhusu shughuli zozote zinazodaiwa kuhusisha uvunjanji wa sheria au kutoa taarifa zinazoanisha watumiaji kwa mamlaka husika pindi wanapombwa kufanya hivyo. Mtoa huduma anayefahamu kuwapo kwa taarifa za kihalifu au zinazovunja sheria analazimika kuiondoa taarifa hiyo kutoka kwenye mfumo wa kompyuta anaoudhibiti, kusimamisha au kusitisha kabisa huduma juu ya kitendo au taarifa hiyo na kuziarifu mamlaka, na kuzipa taarifa sahihi na utambulisho wa watu wanaopewa huduma husika.



- Mtoa huduma ya uwezo wa kuingia kwenye mfumo wa kompyuta (access providers/hosting service providers) hawatawajibika kwa kurusha au kusambaza taarifa kwa ajili ya mtu mwingine. Kwa upande wa mtoa huduma ya kuunganisha tovuti au kutoa uwezo wa kuingia kwenye mfumo wa kompyuta, muhusika hatawajibika kwa makosa ya jinai iwapo ataondoa au kusitisha matumizi ya taarifa baada ya kupokea amri kutoka mamlaka husika au mahakama. Baada ya kutambua uwapo wa taarifa iliyohifadhiwa, mtoa huduma anapaswa kutoa taarifa kwa mamlaka husika haraka iwezekanavyo. Vivyo hivyo, watoa huduma za kuhifadhi data au taarifa (wanaotoa huduma za kusambaza taarifa data au taarifa kwa uhakika zaidi kwa kuzihifadhi ili kuzisambaza kwa watumiaji wengine pale anapoombwa, kwa Kingereza catching providers) na mtoa huduma ya kuunganisha tovuti (wanaotoa huduma ya njia au viungo vya kielektroniki ambavyo vinapofunguliwa kuonesha makabrasha au taarifa, kwa Kingereza hyperlink providers) wanalazimika kuondoa au kusitisha huduma za kupatikana kwa taarifa haraka iwezekanavyo pindi wanapopata maelekezo ya kufanya hivyo kutoka kwa mamlaka husika. [Vifungu vya 40-43]



Notisi ya Kuondoa Taarifa

Kifungu cha 45 kinasema kwamba mtu anaweza, kupitia notisi ya kuondoa maudhui, kumuarifu mtoa huduma kuhusu data, taarifa, au shughuli inayomnyima mpokeaji au mtu mwingine haki ya huduma, vitu au shughuli ambayo ni kinyume cha sheria, au suala lolote linalotekelezwa au kutolewa kinyume cha sheria. Mtoa huduma analazimika kuchukua hatua kuhusiana na notisi ya kuondoa maudhui atakayoipokea.

Athari: Waandishi wa habari na vyombo vya habari vinaweza kuchunguzwa bila ya kujua na kutakiwa kufuata matakwa ya notisi ya kuondoa maudhui kwa taarifa zilizochapishwa mtandaoni zinazoonekana kwenda kinyume cha sheria. Sheria hii inaweza kuathiri haki na uhuru wa watu kujieleza, ikiwemo uchapishaji wa taarifa zenye kuibua hisia za watu na zenye maslahi kwa umma.

Kanuni (za Jumla) za Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2016

Faragha

- Kanuni ya 4 inawataka Watoa Huduma kutoa taarifa binafsi za watumiaji wao kwa “mamlaka husika” pindi wanapoombwa kufanya hivyo.

Athari: Kuna kuingiliwa kwa faragha ya watumiaji kutokana na watoa huduma kulazimika kutoa taarifa binafsi za watumiaji bila ya kuwapo kwa mchakato wa kisheria au utaratibu wa kimahakama. Mtu mmoja mmoja, wakiwemo waandishi wa habari, wafichua uhalifu na wengineo, wanaochapisha taarifa zenye kuibua hisia za watu ambao wasingependa utambulisho wao kufahamika,



wapo kwenye hatari ya kufahamika, kufuatiliwam kutafutwa na kunyimwa au kuvunjwa kwa haki zao nyingine za msingi.

Notisi ya Kuondoa Taarifa

- Kanuni ya 6 na 7 zinaweka mwongozo wa kutoa notisi ya kuondoa taarifa. Mtu yeyote anaweza kupeleka maombi ya notisi ya kuondolewa kwa taarifa fulani pindi anapotambua uwapo wa data au taarifa inayomnyima au kuvunja haki ya mpokeaji au mtu mwingine yeyote, taarifa au shughuli yoyote ya kinyume cha sheria, au jambo lolote linalotendeka kinyume cha sheria. Notisi hizo zinaweza kutolewa na mtu yeyote bila ya kujali kama wana maslahi maalum au uhusika wao kwenye taarifa inayodaiwa kuwa na athari husika.

Athari: Ndani ya saa 24 watoa huduma wanalazimika kutekeleza amri ya kuondoa taarifa au kutoa sababu zinazoeleza kwa nini taarifa kusika isiondolewe. Kupeleka wajibu wa kuthibitisha madai kwa watoa huduma kunaweza kusababisha udhibiti usio wa haki, kwa kuwa watoa huduma wataonelea ni bora kukubaliana na matakwa ya notisi ya kuondoa taarifa kuliko kutathmini ili kuhakikisha kama ni kweli watumiaji wa huduma zao wamejihusisha na shughuli zinazoenda kinyume na sheria. Pale ambapo mtoa huduma ni chombo cha habari, au ana taarifa zinazohusiana na uandishi wa habari, ni dhahiri kwamba taarifa husika zitaguswa ama kuathiriwa na notisi ya kuziondoa.



Sheria ya Takwimu, 2015 (pamoja na marekebisho yaliyofanywa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbalimbali) (Na. 3), 2018 Sheria hii inaunda Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Bodi ya Usimamizi wa Takwimu, na inaeleza kuhusu uratibu wa Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu (NSS).

Vipengele vya msingi ni pamoja na:

Dhima na Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu

- Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni taasisi huru ya umma chini ya Wizara yenye dhamana ya takwimu. Ofisi ya Taifa ya takwimu huzalisha, huratibu, husimamia, na husambaza takwimu rasmi. [Kifungu cha 4-6]
- Ofisi ya Taifa ya Takwimu huratibu Mfumo wa Kitaifa wa Takwimu (NSS) kwa kutoa kanuni za utendaji takwimu rasmi. Kanuni hizo zinaonesha viwango vya weledi zinazoongoza uzalishaji wa takwimu rasmi, vikiwemo ukusanyaji, uchamuzi, na uchapishaji wa takwimu ili kuhakikisha ulinganifu wa jumla katika ubora, utoshelevu, na usahihi wa taarifa za kitakwimu. Ofisi ya Taifa ya Takwimu pia hutoa mwongozo na msaada mwingine kwa watumiaji au watoaji wa takwimu, na hukuza ushirikiano na usawa kati ya watumiaji au watoa takwimu ili kuzuia kudurufiwa kwa jitihada na kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimali chache zilizopo. [Kifungu cha 17]



Ukusanyaji na Uchapishaji wa Takwimu Rasmi

- Takwimu rasmi humaanisha “takwimu zilizozalishwa, kuthibitishwa, kukusanywa (compiled) chini ya mamlaka ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Ofisi ya Taifa ya Takwimu itatathmini wakati na namna ambayo wizara na taasisi zote za serikali zitakusanya na kuchapisha takwimu.
- Takwimu rasmi zitakusanywa tu baada ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuruhusu zoezi hilo, na zoezi husika litafa litatekelezwa na zoezi hilo litekelezwe na watu maalum watakaothibitishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.
- Hata hivyo, kifungu kipya cha 24.A(1) kinaitaka Ofisi ya Taifa ya Takwimu kutoa kinaitaka Ofisi ya Taifa ya Takwimu kupitia na kuruhusu takwimu zote rasmi kabla ya kuzichapisha. Kifungu cha 24.A(2) kinazuia mtu yeyote kuwasiliana taarifa yoyote inayokinzana na takwimu rasmi.
- Kwa mujibu wa kifungu cha 18, ni Mkurugenzi Mkuu pekee anayeweza kuidhinisha, kubadilisha au kusitisha zoezi la ukusanyaji wa takwimu rasmi. Ofisi ya Taifa ya Takwimu ina mamlaka na wajibu wa kuruhusu uchapishaji au uwasilishaji wa taarifa zote zinazohusu takwimu rasmi kwa umma.
- Vifungu vya 25-27 vinahusu ulinzi dhidi ya kuwekwa wazi kwa taarifa, vikiweka



vikwazo kwa utoaji wa taarifa, msamaha kwa utoaji wa taarifa, vikiainisha rekodi za taarifa zinazoweza kuwekwa wazi bila ya kuainisha utambulisho, na namna taarifa hizo zilizowekwa wazi zinavyostahili kutumika.

Athari: Fasili hii mpya na nyembamba “takwimu rasmi” inaonekana kuashiria kwamba takwimu na taarifa zinazotokana na asasi zisizo za kiserikali hazipitia mchakato sawa wa kukubalika kama ilivyo kwa takwimu zinazotokana na taasisi za serikali. Wakati dhana ya “takwimu rasmi” ikifafanuliwa kimamlaka na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, taasisi zisizo za kiserikali, vikiwemo vyo vikiu na asasi za zisizo za kiserikali, ziko huru kuzalisha takwimu pasipo kupata ruhusa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Hata hivyo, takwimu hizo haziwezi “kuwasilishwa” iwapo zinakinzana na takwimu rasmi, hali inayokwaza au kuzuia haki ya kuhoji na uhuru wa kujieleza, na inayoweka mazingira yanayofanana na udhibiti wa moja kwa moja wa taarifa, hata zile zisizozalishwa na serikali. Kwanza, ruhusa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa sasa inahitajika kabla ya kuchapisha takwimu rasmi. Sharti hili linasababisha hatari ya kudhibiti takwimu zisizoivutia Ofisi ya Taifa ya Takwimu au mamlaka mbalimbali za serikali, bila ya kujali ukweli, usahihi na thamani au umhimu wa takwimu husika. Pili, sharti hilo linazuia watu kutowasilisha taarifa yoyote inayokinzana ama kushindana na takwimu rasmi, hali inayoweka watu kwenye hatari ya kuhukumiwa vifungo vya muda mrefu pindi wanapohoji au kubishana kuhusu usahihi wa takwimu rasmi.

Sharti la kupata ruhusa kabla ya kusambaza takwimu rasmi, na katazo la kusambaza takwimu zinazoweza kwenda



kinyume na takwimu rasmi, linazuia uwapo wa mijadala na chambuzi za kitaaluma, mijadala ya kijamii, na mijadala au chambuzi za aina nyingine, kwa kuwa linazuia upatikanaji wa taarifa mbadala. Hali hiyo inasababisha kupatikana kwa taarifa zisizohojika na zitokanazo na chanzo kimoja pekee.

Sheria hii inawataka watu kutoa majibu kamili na yanayojitosheleza kwa maswali yote yaliyoulizwa kwenye fomu na nyaraka zote walizopewa au zilizotumwa kwao. Zaidi ya hapo, watu wanatakiwa kujibu swali au ulizo lolote wanalopelekewa. Matakwa ya sharti hili yanaweza kuathiri haki ya faragha kwa kuwa yanaweza kushurutisha biashara au taasisi kuweka wazi taarifa maalum zinazolindwa kisheria, na watu kuweka wazi taarifa zinazoweza kuwaweka matatani wao wenyewe. Vile vile, ulinzi wa vyanzo vya taarifa kwa waandishi wa habari uko mashakani.

Makosa na Adhabu

- Makosa na adhabu vimeainishwa kwenye Sehemu ya V ya Sheria hii. Makosa hayo ni pamoja na kumiliki, kutumia, au kupata taarifa inayoweza kuathiri thamani ya masoko ya hisa; uchapishaji au uwasilishaji (communication) wa taarifa pasipo mamlaka halali kisheria mbali na zile zinazopatikana kwa mujibu wa utendaji wake wa kazi (ajira/nafasi yake); ukusanyaji [kwa nia ya kuchapisha] (compilation) wa takwimu au taarifa yoyote ya uongo; na kupata au kutaka kupata taarifa ambayo muhusika hana mamlaka ya kuipata. Pia, uchapishaji au uwasilishaji (communication) wa takwimu



rasmi, unaoweza kusababisha upotoshaji wa taarifa yakinifu (facts), ni kosa kwa mujibu wa Sheria hii.

- Ni kosa kushindwa kwa makusudi kutoa maelezo au taarifa za marejesho zinazohitajika na mamalaka husika na adhabu stahiki itatolewa kwa mujibu wa sheria. Vile vile, ni kosa kuharibu, kufuta maandishi au kukata maandishi kwenye nyaraka zozote zenye taarifa kwa mujibu wa Sheria hii bila ya kuwa na mamlaka ya kisheria.
- Vyombo vya habari (vikiwemo vituo vya redio naruninga, magazeti, tovuti na vyombo vingine) vitakavyochapisha au kutangaza takwimu rasmi za uongo au kurusha kipindi chochote kinachohusiana na ukusanyaji wa takwimu kitakazosababisha mtu au watu kukacha, kutoshiriki au kutoa ushirikiano kwenye zoezi la ukusanyaji wa takwimu vitakuwa vimetenda kosa kwa mujibu wa sheria hii.
- Marekebisho ya Sheria hii ya mwaka 2018 yanatambulisha kosa jipya la kuchapisha au kuwasilisha (communicating) takwimu zozote rasmi bila ya kupata ruhusa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Kosa hilo linaweza kusababisha muhusika kupata adhabu ya kifungo cha miaka mitatu gerezani.

Athari: Ujinaishaji wa vitendo fulani unaleta ukakasi kwenye uhuru wa kujieleza na matumizi ya taarifa za kitakwimu.



Kujinaisha uchapishaji na uwasilishaji (communication) wa taarifa zilizopatikana kutokana na majukumu ya ajira halali ya muhusika pasipo muhusika huyo kuwa na mamlaka ya kufanya hivyo ni kuwalenga wafichua uhalifu, waandishi wa habari na taasisi nyingine zinazojihusisha na kufuatilia utendaji serikalini. Pia, kuna adhabu kwa mtu au taasisi yoyote kumiliki taarifa zilizovuja. Hali ya kutokuwapo kwa utetezi wa maslahi ya umma inawaweka wanaovujisha taarifa na wanaochapisha taarifa hizo kwenye hatari ya kutiwa hatiani.

Pia, kuweka kosa la jumla kwa kuzuia watu kutofanya kitu chochote wasichokuwa na mamlaka ya kukifanya kunaleta hatari ya kuwashitaki watu kwa kwa makosa au vitendo butu kimaana na visivyo na ufafanuzi wa wazi kisheria. Vipengele hivi vya kisheria vinaleta ukakasi kwenye uhuru wa kujieleza na kuwa na maoni tofauti.

Kwa ujumla, adhabu zilizowekwa na Sheria hii na sheria nyingine zinaweza kuwa kali mno, hasa kwa kuzingatia uwapo wa adhabu ya kifungo cha chini na faini, adhabu zisizozingatia mazingira magumu yaliyo juu ya uwezo wa wahusika.

Kanuni za Adhabu, Sheria Na. 16, Marejeo ya Mwaka 2002

Makosa ya Jinai Yanayohusu Kashfa

- Kifungo cha 46 kinaeleza kuhusu kosa la kukashifu, na hivyo kujinaisha kashfa.

Athari: Kama ilivyoelezwa hapo awali, kwa ujumla, kitendo cha kujinaisha kashfa kinachukuliwa kama kuweka kikwazo kisicho halali kwa kwa haki na uhuru wa kujieleza na kutoa maoni.



Kosa lisilofafanuliwa Ipasavyo la 'Uvunjifu wa Amani'

- Kifungu cha 123 kinafafanua kosa la kuchochea uadui kati ya makundi mbalimbali, kwa kujinaisha vitendo au maneno yanayochochea uvunjifu wa amani, au hisia za uadui, chuki au nia ovu kati ya makundi tofauti ya kidini, rangi, lugha, makundi ya kieneo au jamii, au inayovuruga au yenye uwezo wa kuvuruga amani na utulivu kwenye jamii.

Athari: Matumizi ya istilahi (maneno) yasiyofafanua dhana za 'uvunjifu wa amani', 'chuki', 'nia ovu' yanaweza kutumika kuwabagua na kuwalenga waandishi wa habari na machapisho yanayokosoa serikali au yanayoibua masuala tete kwenye jamii.

SHERIA ZA USALAMA WA TAIFA ZINAZOZUIA UHURU WA KUTOA MAONI, KUJIELEZA NA VYOMBO VYA HABARI, NA KUPATA TAARIFA

Sheria ya Usalama wa Taifa

Sheria hii inahusika na masuala ya usalama wa nchi ikigusia masuala kama vile ujasusi, uhujumu na shughuli nyingine zenye kuathiri maslahi ya Tanzania.

Vipengele Muhimu

- Kifungu cha 3 kinajinaisha kupata, kukusanya, kurekodi, kuchapisha au kuwasilisha (communicating) nyaraka, makala au taarifa zinazoweza kutumiwa moja kwa moja au



vinginevyo na nchi nyingine au mtu mwenye nia ovu na hivyo kuhatarisha usalama na maslahi ya Tanzania.

- Kifungu cha 5 kinaeleza adhabu kwa kuwasilisha (communicating) au kuvujisha taarifa yoyote ya siri kwa mtu asiyehusika isipokuwa kwa mwenye mamlaka sahihi, au kwa mtu ambaye nchi ina maslahi naye katika kufanya mawasiliano husika. Kutokujua au kutokuweza kufahamu kwamba taarifa aliyoitoa ni ya siri si utetezi unaokubalika kutoka kwa mtuhumiwa.
- Kwa mujibu wa Kifungu cha 13, hakimu anaweza kutoa hati ya kufanya upekuzi itakayowezesha kuingia kwenye jengo au mahali popote, kupekua na kukamata kitu chochote kinachoweza kutumika kama ushahidi kwa kosa lililofanywa chini ya Sheria hii. Katika hali ya dharura, afisa polisi mwandamizi anaweza kutoa amri ya maandishi kwa afisa yeyote wa polisi yenye nguvu inayofanana sawa na hati ya upekuzi inayotolewa na hakimu.
- Kifungu cha 15 kinatoa mamlaka ya kisheria kwa Mkurugenzi wa Mashitaka ya Jinai kuita mtu anayeaminika kuwa na taarifa kuhusiana na makosa yaliyo chini ya Sheria hii, ili kueleza taarifa hiyo kwa afisa wa polisi. Kukaidi au kushindwa kutekeleza agizo hilokunaweza kusababisha muhusika kuhukumwiwa kifungo kisichozidi miaka mitano gerezani.



Sheria ya Kuzuia Ugaidi, 2002

Sheria hii inaeleza hatua madhubuti katika kupambana na ugaidi, kuzuia na kushirikiana na Mataifa mengine katika kukomesha ugaidi.

Vipengele Muhimu

- Kifungu cha 4 cha Sheria hii kinafafanua na kukataza ugaidi.
- Kwa mujibu wa Kifungu cha 28, afisa yeyote wa polisi, pasipo kuwa na hati ya ukamataji, anaweza kumkamata mtu yeyote aliyetenda kosa, anayetenda kosa au anayeshukiwa kwa sababu za msingi kutenda kosa chini ya Sheria hii. Kifungu cha 29 kinaruhusu afisa wa polisi wa cheo fulani kupekua na kukamata pasipo kuwa na hati ya upekuzi au ukamataji, kwenye mazingira ya dharura, au yanayohitaji kuchukuliwa kwa hatua za haraka, ambapo kutofanya hivyo kutasababisha ucheleweshaji utakaopelekea uvunjifu wa amani na utulivu.
- Kifungu cha 30 kinatoa mamlaka kwa Waziri, kwa lengo la kuzuia au kugundua makosa au kuendesha mashitaka ya watuhumiwa chini ya Sheria hii, kutoa mwongozo maalum au wa jumla kwa kadiri atakavyoona inafaa, kwa watoa huduma ya mawasiliano. Mwongozo huo utaonesha muda wa juu ambao mtoa huduma za mawasiliano anaweza kuhitajika kuhitadhi taarifa za mawasiliano.
- Kwa mujibu wa Kifungu cha 31, afisa wa polisi anaweza, kuiomba mahakama, kwa maslahi ya



nchi (maslahi ya upande mmoja), kutoa amri ya kuingilia mawasiliano kwa nia ya kupata ushahidi wa kutendeka kwa kosa chini ya Sheria hii. Mahakama inaweza kumuamuru mtoa huduma za mawasiliano kuingilia na kuhifadhi mawasiliano yaliyotajwa au yaliyopokelewa au kutumwa na mtoa huduma huyo, au inaweza kumruhusu afisa wa polisi kuingia kwenye eneo lolote na kufunga kifaa chochote cha kuingilia na kuhifadhi mawasiliano, na kuondoa kifaa hicho kutoka eneo hilo, kwa ridhaa ya maandishi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu ikionesha sababu za msingi za kuamini kwamba taarifa zinazohitajika zinapatikana kwenye mawasiliano hayo.

- Kifungu cha 33 kinatoa mamlaka kwa Polisi kukamata mali inayoshukiwa, kwa sababu za msingi, kutumika kwenye kutenda kosa la ugaidi chini ya Sheria hii, pasipo kujali uwapo wa mashauri yaliyofunguliwa chini ya Sheria hii au la.

Sheria ya Intelijensia na Huduma za Usalama, 1996

Sheria hii inaunda Idara ya Usalama wa Taifa (TISS) na itahusu masuala yanayohusiana na usalama.

Vipengele Muhimu

- Idara ya Usalama wa Taifa inaundwa kama kitengo cha Serikali chini ya Ofisi ya Rais. [Kifungu cha 4] Mkurugenzi Mkuu ana mamlaka ya kutoa amri, kudhibiti, kuelekeza, usimamizi wa jumla na utawala wa Idara ya



Usalama wa Taifa kwa mujibu wa mamlaka aliyepewa na Rais na mwongozo kutoka kwa Waziri. [Kifungu cha 10]

- Kazi za TISS zinajumuisha kukusanya na kutathmini taarifa za kiuchunguzi zinazohusu masuala ya usalama na kuziwasilisha kwa watu au vyombo husika. Sheria inaeleza wazi kwamba Idara ya Usalama wa Taifa haina mamlaka ya kufuatilia nyendo za mtu au watu (surveillance) kwa kuwa tu watu hao wameshiriki kwenye maandamano halali au kuwa na maoni na mitazamo tofauti juu ya masuala yanayogusa au kuhusu sheria au Serikali ya Tanzania.
- Kwa mujibu wa kifungu cha 14, Idara ya Usalama wa Taifa imepewa mamlaka ya kukusanya kwa kufanya uchunguzi au vinginevyo, kwa kiwango kinachohitajika tu (strictly), na kuchambua na kutunza taarifa za kiuchunguzi kuhusu shughuli zinazoshukiwa kutishia usalama wa Tanzania. Kifungu cha 5 kinaipa mamlaka Idara ya Usalama wa Taifa kuchunguza mtu yeyote au kikundi cha watu ambaye au ambacho idara hiyo inamshuku au inakishuku kuhatarisha usalama wa nchi.
- Kifungu cha 16 kinazuia kutaja (kuchapisha au kutangaza), pasipo ridhaa ya maandishi kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya intelijensia na usalama (na iwapo hakutakuwa na mtu aliyeteuliwa kushika nafasi hiyo kwa



wakati huo, Rais atatoa ridhaa hiyo), jina au utambulisho wa mtu yeyote, isipokuwa Mkurugenzi Mkuu, anayehusiana na Idara ya Usalama wa Taifa.

- Pia, sheria inakataza kutoa taarifa zinazoweka wazi kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja utambulisho wa watu walioajiriwa au kuhusika katika shughuli mbalimbali za siri. [Kifungu cha 20]

Athari za Sheria za Usalama kwa Vyombo vya Habari

- Sheria zinazohusu usalama wa Taifa kwa ujumla zinakataza uchapishaji na uwasilishaji (communication) wa taarifa za aina fulani na hutoa mamlaka pana kwa vyombo vya maafisa wanaosimamia sheria kuingilia kati, kupekua na kukamata taarifa, vifaa nk. vinavyokisiwa kuhusika kwenye vitendo vya uvunjifu wa sheria. Aghalabu, hilo hufanyika pasipo kuwapo au kufuata utaratibu wa kisheria au mchakato wa kimahakama katika kutoa au kuidhinisha amri husika.
- Waandishi wa habari na watendaji wengine kwenyevyombo vya habari, hasa wanapojitahidi kufuatilia uwajibikaji Serikalini, hukutana na hatari kubwa ya kuchunguzwa kwa kufuatiliwa nyendo zao (surveillance), na vifaa vyao kutwaliwa. Kwa kisingizio cha usalama wa taifa, waandishi wa habari, watendaji wengine kwenye vyombo vya habari, au watu wengine wa upande huru (kama vile watoa huduma)



wanaweza kulazimishwa kuweka wazi taarifa na vyanzo vya habari vinavyostahili kuwa siri, hali inayoweza kuharibu utendaji kwenye tasnia ya habari.

- Zaidi ya hapo, taarifa binafsi za utambulisho wa waandishi wa habari na watumiaji wa mitandao ya jamii zinaweza kuwekwa wazi na watoa huduma za mawasiliano pindi mamlaka zinapowalazimisha watoa huduma hao kufanya hivyo.

SURA YA IV

KUPAMBANUA MISINGI YA KISHERIA –
KINGA NA MIKAKATI



MCHAKATO WA KUDAI HAKI KISHERIA

Waandishi wa habari na watendaji wengine kwenye tasnia ya habari wana wajibu wa kutambua sheria zinazoweza kuwaathiri wao wenyewe, kuathiri machapisho yao na shughuli zao, kwenye mtandao wa intaneti na njeya mtandao. Wanatakiwa pia kuelewa kinga mbalimbali zinazotolewa na Katiba, mikataba mbalimbali ya ya kimataifa na kikanda, miiko pamoja na kanuni mbalimbali za maadili na utendaji. Kama ilivyokwishasemwa awali, vipengele vingi vya sheria mbalimbali zilizojadiliwa kwenye Kijitabu hiki vinaashiria kuvunja ama kukiuka haki ya msingi ya uhuru wa kujieleza, kutoa maoni, na kusambaza na kupata taarifa. Kwenye mazingira kama hayo, ni muhimu kwa mtu kutumia mbinu ya Jaribio la Sehemu Tatu kutathmini uhalali wa kikwazo kinachomkabili katika kutekeleza majukumu yake.

Inapogundulika kwamba kikwazo kilichopo si halali, mtu au taasisi iliyothiriwa na kikwazo hicho ina haki ya kwenda mahakamani kutafuta kinga au fidia kwa mujibu wa sheria. Wanasheria, vyombo na taasisi zinazohusika na masuala ya habari, na watetezi wa haki za binadamu nchini Tanzania wamewahi kwenda mahakamani za ndani, za Afrika Mashariki na barani Afrika kupinga vipengele mbalimbali vya sheria mbalimbali vinavokandamiza uhuru wa habari, maoni na kujieleza. Yafuatayo hapa chini ni



baadhi ya mashauri muhimu yaliyowahi kushughulikiwa na mahakama mbalimbali:

Ngazi ya Kitaifa

Unaweza kusoma zaidi kuhusu mashauriyaliyowasilishwa kwenye mahakama za ndani na kanda kwa kufungua viungo (tovuti) vifuatavyo:

Maktaba ya Mahakama ya Afrika Mshariki: <http://eacj.org/>

Mashauri Yaliyofikishwa Mahakama ya Rufaa ya Tanzania: <http://www.saflii.org/tz/cases/TZCA/>

Mashauri Yaliyofikishwa Mahakama Kuu ya Tanzania: <http://www.saflii.org/tz/cases/TZHC/>

Tovuti ya Baraza la Habari Tanzania: <https://mct.or.tz/index.php/media-bills>

Mchakato wa Kudai Haki Kikanda na Kimataifa

Njia ya kutafuta haki kwa kupitia vyombo na mikataba ya kikanda na kimataifa, isipokuwa katika mazingira machache, hulazimu pale mifumo ya ndani ya nchi – kama vile mfumo wa mahakama – imekwishafuatwa kikamilifu katika ngazi zote, au pale ambapo mwathirika atathibitisha kukosekana au kutokuwapo kwa mchakato huo wa kisheria kwenye mifumo ya ndani ya nchi.

- Kikanda, mtu yeyote anaweza kuwasilisha malalamiko ya kukiukwa kwa haki zake dhidi ya Nchi kwenye **Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Umoja wa Afrika**. Mkataba wa Haki za Binadamu na Watu wa Umoja wa Afrika umeweka utaratibu wa



kuwasilisha maombi kwenye Tume, ikiwemo vigezo vya kukubaliwa kwa malalamiko yanayowasilishwa. Pindi Tume inapotoa maamuzi kuhusu malalamiko fulani kwa kuzingatia uzito wa ushahidi uliowasilishwa, hutoa uamuzi wa mwisho (mapendekezo). Maamuzi ya Tume hukosa nguvu ya kisheria kwenye nchi Nchi husika hadi pale unapopitishwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika. Tume inweza kuziomba (yenyewe au kwa kupokea maombi ya kufanya hivyo) nchi zinazoshutumiwa kukiuka haki zilizoainishwa kuchukua hatua za mpito kuzuia madhara yasiyorekebishika kwa waathirika, mara tu baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa mwathirika au mtuma maombi husika. Utaratibu wa hatua za mpito unazitaka Nchi husika kupeleka mrejesho kuhusu hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa ndani ya siku kumi na nne baada ya kupelekwa kwa ombi husika.

- Pia, mtu mmoja mmoja anaweza kupeleka malalamiko rasmi kupitia **Utaratibu Maalum wa Tume ya Afrika na Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa** (kimsingi, lakini si kipekee, kwa kupitia Waangalizi Maalum wa Uhuru wa Haki Kujieleza pamoja na Watetezi wa Haki za Binadamu) wakizituhumu Nchi kukiuka haki zao za msingi. Waangalizi hao Maalum



huwasilisha malalamiko hayo kwa Nchi zilizotajwa, ambazo kwa kawaida hutakiwa kujibu tuhuma zinazowakabili.

- **Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu** ina mamlaka ya kisheria ya kushughulikia mashauri na migogoro iliyowasilishwa kwake kuhusu fasili ya na matumizi ya Mkataba wa Haki za Binadamu na Watu wa Umoja wa Afrika. Watu wanaweza kuwasilisha mashauri dhidi ya Nchi wanayoilalamikia, yaani nchi iliyoridhia Mkataba ulianzisha na kuweka azimio linalotambua mamlaka ya Mahakama hiyo kupokea mashauri kutoka kwa watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Tanzania imeridhia Mkataba huo na inalitambua azimio hilo. Maamuzi ya Mahakama ya Afrika yana nguvu ya kisheria kwenye Nchi Wanachama.
- **Mahakama ya Afrika Mshariki** ina mamlaka ya juu ya fasili na matumizi ya Mkataba wa Jumua ya Afrika Mshariki. Kwa sasa, Mahakama hii haina mamlaka ya kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu mashauri yanayohusu masuala ya haki za binadamu, lakini mamlaka hayo yanaweza kujumuishwa kwa maamuzi ya Baraza la Mawaziri.



KUFUATA MAADILI YA TAALUMA YA UANDISHI WA HABARI

Kama ilivyokwishajadiliwa tangu mwanzo, japokuwa waandishi wa habari na watendaji wengine kwenye vyombo vya habari wana haki ya kutumia haki yao ya kujieleza kwa uhuru na kupata na kusambaza taarifa, pia wana majukumu fulani, ikiwemo wajibu wa kufuata maadili na viwango vya taaluma ya uandishi wa habari wakati wa kutekeleza majukumu yao. Viwango na kanuni hizo zinajumuisha kutoa habari za kuaminika, sahihi na zenye ukweli, na kuwapo kwa uadilifu na uhuru katika kutekeleza majukumu ya uandishi wa habari. Iwapo waandishi watafuata kanuni hizi wakati wa kutekeleza majukumu yao, na kuhakikisha kwamba taaluma yao haitiwi doa kutokana na uzembe au vitendo vya makusudi, itakuwa vigumu kwao kuwindwa au kutafutiwa makosa, na jamii itawaunga mkono zaidi pale watakaposhitakiwa bila pasipo haki. Baraza la Habari Tanzania limetoa Kanuni za Maadili kwa Waandishi wa Habari kwa Wanataaluma wa Habari. Baadhi ya kanuni za msingi zimeainishwa hapa chini:

- **Ukweli na Usahihi wa Taarifa:** Epuka kuonesha upendeleo, na mar azote hakikisha kwamba unatenda haki kwa pande zote zinazohusika kwenye habari unayoiandaa. Sahihisha na omba msamaha mara unapogundua kuchapishwa au kutangazwa kwa habari isiyo sahihi au yenye taarifa potofu.



- **Haki ya Kujibu:** Mara zote, wahusika wa habari fulani wanastahili kupewa fursa ya kujibu jambo linalowahusu au kuwagusa kabla ya kuchapishwa au kutangazwa kwa habari husika.
- **Faragha:** Pata ridhaa ya muhusika kabla ya kuchapisha au kutangaza habari kuhusu maisha binafsi ya mtu yeyote, isipokuwa iwapo kuna sababu ya msingi inayohusu maslahi ya umma kwenye habari unayoandaa. Hata watu wanaoshika madaraka kwenye ofisi za umma wana haki ya faragha, isipokuwa iwapo taarifa husika itaathiri utendaji ama uwapo wao kwenye nafasi ya uongozi wa umma wanayoishikilia au wanayoitafuta.
- **Vitisho:** Tafuta habari kwa kutumia njia za kawaida kwa kadiri inavyowezekana. Hairuhusiwi kutafuta habari kwa njia ya vitisho, kumchafua mtu, uongo, ujasusi, au vitisho vya aina yoyote nyingine, na kufanya hivyo kunaweza kusababisha jinai kwa muhusika.
- **Ubaguzi:** Epuka kutoa kauli zisizofaa au kufanya ubaguzi kwa misingi ya rangi, umri, jinsia, imani, ulemavu, jografia, maumbile au hadhi ya kijamii. Tumia lugha isiyokuwa na ubaguzi, inayozingatia usawa wa kijinsia na inayoheshimu haki na utu wa watu unaowazungumzia kwenye habari unayoiandaa.



- **Watoto:** Pata ridhaa ya wazazi au walezi iwapo utahitaji kufanya mahojiano au kuwapiga picha watoto wenye umri chini ya miaka 16. Majina ya watoto, hata watoto wanaohusika kwenye mashauri mahakamani, hayapaswi kuwekwa wazi. Pia, si sahihi kueleza kwa undani vitendo vya ngono vinavyohusisha watu wazima na watoto wadogo.
- **Wahanga wa unyanyasaji wa kingono:** Utambulisho wa wahanga wa vitendo vya shambulio la ngono ni lazima ulindwe bila ya kuwekwa wazi. Hii ni pamoja na kuchukua hatua za kutotoa taarifa zitakazoweza kuonesha au kuashiria utambulisho huo.
- **Kueleza kuhusu vitendo vya ngono:** Ili kutunza heshima ya jamii, epuka kueleza kwa undani na waziwazi kuhusu vitendo vya ngono.
- **Uhalifu:** Epuka kusifia uhalifu au tabia inayochochea vurugu pindi unaporipoti kuhusu matukio ya uhalifu. Pia, epuka kuhusisha familia za wanaotuhumiwa kwa uhalifu na uhalifu uliotokea.
- **Huzuni na simanzi:** Kuonesha busara na kujali ni vigezo muhimu wakati wa kutafuta na kuandika ama kutangaza habari kuhusu majanga na matukio ya kuhuzunisha. Usiongeze machungu kwa wahanga, na epuka kuwapa shinikizo ili kufanya mahojiano na waathirika hao.



- **Ushawishi na maslahi binafsi:** Epuka ushawishi usiostahili kutoka kwa vyanzo vya habari. Kamwe usiruhusu maslahi binafsi au ya familia kuingilia majukumu yako ya kitaaluma. Kuwa macho na, pia epuka, mgongano wa maslahi.
- **Vyanzo vya siri (vya taarifa):** Waandishi wa habari wana wajibu wa kimaadili kulinda vyanzo vya siri vya taarifa wanazozipata.
- **Kuzuia (kuficha) taarifa:** Usizuie taarifa muhimu au habari yoyote isipokuwa iwapo kuna sababu za msingi zinazohusu maslahi ya umma za kusababisha kufanya hivyo.
- **Uhuru wa vyombo vya habari:** Wakati wote, fanya kazi kwa kutetea uhuru wa vyombo vya habari, na uwe macho na wanaotumia uhuru huo kwa maslahi yao binafsi.

KUJENGA UWEZO WA KISHERIA, MAADILI YA KITAALUMA NA USALAMA BINAFSI NA WA KITAASISI

Kwenye nchi nyingi, watendaji mbalimbali kwenye vyombo vya habari huchukuliwa kuwa ni watu walio kwenye hatari kubwa ya kushambuliwa na Dola (na wakati mwingine) vyombo visivyo vya dola. Kutokana na hilo, kuna umuhimu mkubwa kuelewa na kushughulikia masuala ya usalama na ulinzi wa wanahabari, ili kutengeneza na kutekeleza mikakati thabiti kwa kuhakikisha usalama wa



wanahabari. Kuna hatua mbalimbali za kuchukua katika kushughulikia usalama binafsi na wa kitaasisi na pia katika kukabiliana na hatari:

- i. Fahamu muktadha:** Mambo muhimu ya kutazama ni pamoja na mazingira ya kisiasa, mazingira ya kijamii na kiutamaduni, masuala ya kiteknolojia, misingi ya kisheria, na vigezo vingine vya kimazingira.
- ii. Andaa sera ya usalama:** Hizi ni kanuni za jumla, misingi na miongozo ya kufuata katika kuhakikisha usalama.
- iii. Andaa mpango wa usalama:** Huu ni waraka unaojumuisha hatua za kuzuia na kushughulikia mfumo wa ulinzi ili kuborsha hali ya ulinzi binafsi na wa kitaasisi. Mpango huu ni namna ya utekelezaji wa sera yako ya usalama. Hatua za kufuata katika kuandaa mpango wa usalama hujumuisha:
 - a. Orodhesha hatari zilizopo
 - b. Pembua ili kufahamu madhara yanayohusiana na kila hatari
 - c. Ainisha uelewa na uwezo unaohitajika katika kuzuia hatari husika kutokea
 - d. Ainisha vitu au rasilimali zinazohitajika katika kutekeleza mpango huo
 - e. Weka muda maalum na majukumu yanayotakiwa kutekelezwa katika muda



husika kwa kila hatua iliyoainishwa

- f. Tenga muda wa kufanya marejeo, kutafakari na kuboresha mpango wa usalama

Usalama mtandaoni ni dhana muhimu katika kushughulikia usalama binafsi na wa kitaasisi kwenye tasnia ya habari katika Karne ya 21. Kazi nyingi kwenye vyombo vya habari hufanywa kielektroniki kwa kutumia kompyuta na vifaa vingine vya kielektroniki. Teknolojia hubeba hatari za namna fulani zinazoweza kutumiwa vibaya na kuwaathiri watumiaji. Ni muhimu kwa watendaji kwenye tasnia ya habari kuelewa namna ya kuimarisha usalama wa vifaa wanavyotumia, taarifa, mitandao, na akaunti za watumiaji.

- i. **Kutambua hatari:** Kutambua hatari kunahitaji kufanya tathmini kwa lengo la kutambua kitu linalohitaji kulindwa, kulindwa dhidi ya hatari gani, uwezekano wa kitu hicho kushambuliwa, madhara yanayoweza kutokea kwa kutolinda kitu hicho, na kiwango cha jitihada zilizopo katika kuzuia mashambulizi dhidi ya kitu hicho. Kufahamu undani hatari iliyopo husaidia katika kutafuta suluhisho sahihi kwa tatizo husika.
- ii. **Vitu vya msingi katika usalama wa vifaa vya kielektroniki:** Hivi hujumuisha kuhuisha programu za kupambana na virusi vya kompyuta, kuepuka kupakua makabrasha yenye mashaka mtandaoni, kutazama dalili za kuingiliwa kwa mfumo wa kompyuta, kupata programu za kompyuta kutoka mahali sahihi



– ikiwezekana, programu zitoke moja kwa moja kwa mtengenezaji.

- iii. Usalama wa taarifa kwenye vifaa vya kielektroniki:** Kuficha taarifa (encryption) kwa kutumia mbinu maalum kwenye kompyuta [usimbaji fiche] husaidia kulinda taarifa dhidi ya mashambulio na kuzifanya zisionekane hata kama kompyuta au kifaa husika kitaibwa.
- iv. Usalama wa taarifa kwenye mtandao wa intaneti:** Tumia njia salama za mawasiliano, kama vile programu zisizoruhusu mtu asiyehusika kuona ama kuingilia mawasiliano hayo (end-to end encryption) Epuka udhibiti wa mtandao wa intaneti, hasa kutumia viungo vinavyotoa ruhusa ya kuweza kuingia kwenye tovuti zilizozuiwa, tengeneza Jina Tofauti la Utambulisho Mtandaoni (Domain Name Service – DNS) kama vile zinazotolewa na mtandao wa Google ili kuepuka kufuatiliwa kwa utambulisho wako binafsi wa mtumiaji wa mtandao, na tumia Mtandao Binafsi (VPN) ili kulinda taarifa dhidi ya kuingiliwa kati.
- v. Usalama wa akaunti ya mtumiaji:** Hakikisha usalama wa akaunti yako kwa kuweka neno-siri lililo imara, epuka kutumia neno-siri linalofanana, na tumia njia ya uhakiki yenye hatua mbili (two-step verification).
- vi. Usalama kwenye simu za mkononi:** Tumia programu ya kufunga kioo cha simu, hakikisha



simu yako na programu zilizomo zinakwenda na wakati, epuka kuweka programu (Apps) kutoka sehemu zisizo rasmi, zima uwezo wa kuonekana na kutambulika kwenye programu ya Bluetooth. Fuata mapendekezo yaliyotolewa hapo juu kuhusu usalama wa taarifa na simu, pakua programu kama vile 'Panic Button', 'CameraV', na nyingine zinazosaidia kuhakikisha usalama.

KUTOA TAARIFA NA KUWEKA KUMBUKUMBU YA VITENDO VYA UKIUKWAJI WA HAKI

Usimamizi ama ufuatiliaji wa haki za binadamu ni dhana inayotumika kurejelea ukusanyaji, uhakiki, na matumizi ya taarifa katika kushughulikia matatizo yanayohusiana na haki za binadamu. Ufuatiliaji ni njia ya kuboresha ulinzi wa haki za binadamu na unalenga kuongeza uwajibikaji wa Dola katika kulinda haki za binadamu. Ufuatiliaji wa haki za binadamu unahitaji umakini katika kukusanya taarifa sahihi kwa kupitia njia za kuhoji, kufuatilia, na kuchambua mapitio na mwenendo wa matukio mbalimbali, pamoja na utambuzi wa mienendo na vitendo mbalimbali. Kukusanya taarifa sahihi, timilifu, na zisizoegemea upande wowote ni jambo muhimu kwa kuwa kufanya hivyo kunawezesha kutambua matatizo kwa uhakika. Mchakato huo pia huwezesha kutambua chanzo cha tatizo na kutafuta suluhisho. Ushahidi na taarifa zinazoweza kuthibitika na pia husaidia katika kufanya kazi na vyombo vya serikali na kuwezesha utetezi wa mabadiliko ya sera, sheria, na utendaji.



Kanuni tatu huongoza utaratibu wa kuthibitisha taarifa pindi zinapokusanywa:

- i. kuaminika kwa chanzo cha taarifa,
- ii. kuendana na taarifa zilizokusanywa kupitia vyanzo huru vya taarifa, na
- iii. namna taarifa husika inavyoendana na muktadha uliopo

Taarifa iliyothibitishwa hutumika kutengeneza ripoti za aina mbalimbali na pia huwa ni msingi kuchukua hatua za kurekebisha hali iliyo kwenye eneo fulani.

Press Freedom Violations Register (PFVR)

Mwanzoni mwa mwaka 2012, Baraza la Habari Tanzania lilianzisha rejesta ya kutunza taarifa zinazohusu ukiukwaji wa haki ya uhuru wa vyombo vya habari nchini Tanzania, inayojulikana kama Rejesta ya Ukiukwaji wa Uhuru wa Vyombo vya Habari (PFVR). Rejesta hiyo hufuatilia ukiukwaji wa haki za uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza nchini Tanzania. Rejesta hiyo:

- Hutengeneza taarifa muhimu za kitakwimu kwa lengo la kusisitiza, kulinda na kutetea uhuru wa habari na njia nyingine za kujieleza na mawasiliano ya jamii.
- Hutoa ushahidi madhubuti wa kiwango cha uhuru wa habari ambacho kinachoakisi mazingira ambayo vyombo vya habari nchini Tanzania vinafanya kazi;
- Husaidia watendaji kwenye vyombo vya habari kuelewa mwenendo wa ukiukwaji wa haki ya uhuru wa habari na maoni;



- Ni jukwaa linaloweza kuweka kumbukumbu na kufanya uchunguzi wa ukiukwaji mkubwa wa haki ya uhuru wa habari na kutoa maoni; na
- Hufanya kazi kama nyenzo muhimu muhimu katika utetezi wa haki ya uhuru wa vyombo vya habari, kujieleza, na mabadiliko ya sheria zinazohusu taarifa.

Rejesta hiyo inaweza kupatikana kwenye kiungo kifuatacho mtandaoni: <https://pressviolations.or.tz/#/views/map>

Njia nyingine

Majukwaa mbadala yanayoweza kutumika kutoa taarifa juu ya ukiukwaji wa haki za uhuru kujieleza na wa vyombo vya habari yanahusisha kuandika malalamiko au kupiga simu kwenda Baraza la Habari Tanzania kwa hatua zaidi.

UTETEZI NA KUJIHUSISHA KATIKA KUDAI MABADILIKO

Inapowezekana, ni muhimu kwa watendaji kwenye vyombo vya habari, wanasheria, na watetezi wa haki za binadamu kufanya kazi kwa ukaribu na Serikali na kujadili wasiwasi wao na kudai mabadiliko na kuimarishwa kwa taasisi. Kwa kuzingatia misingi ya kibunge ya kubadili sheria, malengo muhimu ni:

- Watungasera (wakiwemo Rais, Wabunge na wataalam)
- Watunga sheria/wabunge
- Tume ya Kurekebisha Sheria



- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, zikiwemo idara za sera na uandishi
- Taasisi za Kitaifa za Haki za Binadamu

Mtandao imara wa asasi za kiraia huimarisha matokeo ya utetezi wa haki za msingi, hasa iwapo mtandao huo utajumuisha wawakilishi kutoka pande na taaluma mbalimbali. Fikiria kujumuisha:

- Asasi za kiraia kwenye ngazi ya taifa na ngazi ya jamii
- Wadau kutoka tasnia ya habari
- Vyama vya kitaaluma, kama vile Vyama vya Wanasheria na Vyama vya Mawakili
- Vyama vya wafanyakazi
- Taasisi za dini
- Makampuni
- Vyuho vikuu na wanataaluma
- Mashirika ya kikanda
- Mashirika ya maendeleo ya kimataifa

Kutumia mifumo ya kikanda na kimataifa

Watendaji mbalimbali kwenye vyombo vya habari wanaweza kubeba majukumu ya utetezi kwenye ngazi za kikanda na kimataifa, kwa kuiarifu mifumo mbalimbali ya utetezi wa haki za binadamu kuhusu hali ya uhuru wa vyombo vya habari na kutoa maoni ilivyo nchini Tanzania.



- **Kamati Maalum ya Umoja wa Mataifa ya Mapitio Jumuishi Maalum ya Haki za Binadamu (Universal Periodic Review):** Huu ni mfumo unaotumiwa na Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa kufanya mapitio ya hali ya haki za binadamu kwenye nchi 193 Wanachama wa Umoja wa Mataifa kila baada ya miaka mitano. Matokeo ya mapitio hayo huoneshwa kwenye taarifa ya mwisho ya Kikundi Kazi ikijumuisha orodha ya mapendekezo yanayoitaka Serikali kutekeleza kablaya kufika kwa kipindi kingine cha mapitio, yaani ndani ya miaka mitano. Japokuwa huu ni mchakato unaohusisha mamlaka za Nchi, asasi za kijamii (CSOs) zinaweza kushiriki kwa njia tano tofauti: (i) kushiriki kupitia mikutano ya kitaifa inayoendeshwa na Nchi ya kukusanya maoni mbalimbali wa wadau, (ii) kutuma taarifa kivuli kuhusu hali ya haki za binadamu kwenye nchi husika, (iii) kuzungumza na wahusika kwenye Kikundi Kazi wanaoendesha mchakato wa mapitio, (iv) kuwasilisha Taarifa ya Wadau (shadow report) kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, na (v) kufuatilia na kushiriki katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa wakati wa mapitio.
- **Taarifa Kivuli Kwenda Kwa Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu ya Umoja wa Afrika:** Nchi huwasilisha taarifa hizi kila baada ya miaka miwili, mchakato unaowezesha Tume hiyo kufuatilia utekelezaji wa matakwa



ya Mkataba wa Afrika kuhusu haki za binadamu na watu, na kuainisha changamoto mbalimbali katika kufikia utekelezaji wa haki zilizoainishwa kwenye Mkataba huo. Nchi hupata fursa ya kujitathmini kuhusu mafanikio waliyoyapata na changamoto zilizopo katika kufikia utekelezaji wa matakwa ya haki za binadamu kwenye viwango vinavyostahili. Asasi za kiraia zinaweza kutuma taarifa sambamba (parallel report) zinazoeleza mtazamo wao kuhusu changamoto zilizopo, na hatua gani zichukuliwe na Nchi husika katika kurekebisha hali iliyopo na kushughulikia changamoto matatizo hayo. Watendaji kwenye vyombo mbalimbali vya habari nchini Tanzania wanaweza kuwasilisha taarifa zinazofafanua changamoto mbalimbali za kisheria wanazokabiliana nazo katika utendaji wao na kupendekeza masuluhisho kwa kila changamoto husika.

MIFUMO SAIDIVU

Msaada wa Kisheria

- Uchunguzi
- Utetezi
- Mfuko wa Kusaidia Vyombo vya Habari

Msaada wa Kisaikolojia (Psychosocial Support)

- Ushauri nasaha
- Uokoaji kutoka mazingira hatarishi

SURA YA V

REJEA MUHIMU



Tamko la Kimataifa la haki za Binadamu

<http://www.un.org/en/universal-declaration-human-rights/>

Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa

<https://www.ohchr.org/en/professionalinterest/pages/ccpr.aspx>

Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, Ufafanuzi wa Jumla Na. 34 (UN Human Rights Council, General Comment No. 34)

<https://www2.ohchr.org/english/bodies/hrc/docs/gc34.pdf>

Taarifa ya Mwangalizi Maalum wa Umoja wa Mataifa kwenye kulinda haki na uhuru wa kutoa maoni na kujieleza

<https://www.ohchr.org/en/issues/freedomopinion/pages/opinionindex.aspx>

Kamati Maalum ya Umoja wa Mataifa ya Mapitio Jumuishi Maalum ya Haki za Binadamu (Universal Periodic Review – UPR)

<https://www.ohchr.org/en/hrbodies/upr/pages/uprmain.aspx>

Tume ya Haki za Binadamu na Watu ya Umoja wa Afrika

<http://www.achpr.org>



Taarifa ya Mwangalizi Maalum wa Tume ya Afrika Kuhusu Uhuru wa kujieleza (ACHPR Special Rapporteur on Freedom of Expression)

<http://www.achpr.org/mechanisms/freedom-of-expression/>

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu:

<http://www.african-court.org/en/>

Kanuni za Maadili kwa Wanataaluma wa Habari, Baraza la Habari Tanzania, (Toleo la 2016)

<https://mct.or.tz/index.php/tutorials/code-of-ethics-for-professionals>

Mahakama ya Afrika Mashariki: Mwongozo kwa Watumiaji (Septemba 2013) (East African Court of Justice: Court Users' Guide)

<http://eacj.org/wp-content/uploads/2013/11/EACJ-Court-Users-Guide-September-2013.pdf>

Admissibility of Complaints before the African Court: Practical Guide, FIDH, (June 2016)

https://www.fidh.org/IMG/pdf/admissibility_of_complaints_before_the_african_court_june_2016_eng_web-2.pdf

Centre for Human Rights, A Guide to the African Human Rights System, Pretoria University Law Press (2016)

<http://www.corteidh.or.cr/tablas/31712.pdf>

Stand Up! Security guide for human rights defenders in Africa, DefendDefenders, 2017

<https://www.defenddefenders.org/wp-content/uploads/2017/09/StandUpfeb.pdf>



Don't Shoot the Messenger! Journalists as human rights defenders in the East and Horn of Africa, DefendDefenders, 2017

<https://www.defenddefenders.org/wp-content/uploads/2017/11/DontShootTheMessenger.pdf>

Defending Human Rights: A Resource Book for Human Rights Defenders (2nd Ed.), DefendDefenders, 2012

http://www.defenddefenders.org/wp-content/uploads/2011/07/EHAHRPD_Resource_book_ENG.pdf

Professional Training Series No. 7: Training Manual on Human Rights Monitoring, OHCHR 2001

<https://www.ohchr.org/Documents/Publications/training7introen.pdf>

Manual on Human Rights Monitoring: An introduction for Human Rights Field Officers, Norwegian Centre for Human Rights, 2008

<https://www.jus.uio.no/smr/english/about/programmes/nordem/publications/manual/>

